# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja la tatu na la nne

Mfululizo wa A
Masomo ya kwanza hadi sita

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya “Wakati na Biblia/Bibletime”, “Maisha Mapya/New Life” na “Wakusanyaji/Gleaners” kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wamechukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wakufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa na vikundi mbalimbali kutoka makanisa na shule mbalimbali ambavyo vimezingatia mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na yanamruhusu mwanafunzi kuyatumia kwa muda mrefu hadi atakapotimiza umri wa miaka ishirini. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (chini ya miaka mitano), miaka mitano hadi saba, miaka nane hadi kumi, miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu na miaka kumi na minne hadi kumi na sita. Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 6). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongonzo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwa mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES

**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo wa kufundisha umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo wa kufundisha katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya daraja la tatu na la nne kwa watoto wenye umri wa wastani wa miaka 11-16.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kwa kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Hatupendi kutoa shinikizo na kutokuwapa waalimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri –** Waalimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kukamilisha somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza –** Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno 'Tunajifunza kuwa' ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kukamilisha somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Waalimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi –** Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha –** Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba waalimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Kuonesha –** Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Viunga (links) maalum vya tovuti ya Free Bible Images kwa ajili

ya Masomo yote ya daraja zote na mfululizo wote wa Wakati na Biblia yanapatikana kwa barua pepe kutoka kwenye ofisi ya BES. Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

- **Rejelea Somo –** Tunashauri pale inapowezekana pawepo majaribio au vitendo ili kurahisisha ujifunzaji, na kama njia ya kufanya marudio ya habari.
- **Liishi Somo –** Sehemu hii imebeba kichwa cha habari, 'kwa namna gani somo hili linatupa changamoto' na pia mapendekezo kadhaa ya kazi inayoweza kufanywa kwa vikundi na majibu ya mtu binafsi kwa changamoto ya somo.

## Kufundisha Mstari Muhimu

1) Mstari unafaa kuandikwa kwenye karatasi au ubaoni na baadhi ya maneno kuondolewa huku watoto wakirudia ule mstari hadi pale maneno yote yatakapoondolewa na watoto kuurudia mstari bila kuangalia maneno.
2) Ili kuwaanzishia watoto Mstari muhimu, mwalimu anaweza kutumia:
   a) Njia ya Hangman yenye vikundi viwili (2 teams) – Unaweza kuwapa watoto baadhi ya nafasi za herufi za ule Mstari muhimu bila herufi zenyewe – Watoto watachagua herufi wanazozitaka mpaka mtu atakapoweza kuuona Mstari muhimu.
   b) Njia ya Sword Drill – watoto wanakuwa na Biblia na wote wanashindana kutafuta mstari huo wa Biblia na atakayeupata wa kwanza ataruhusiwa kuusoma kwa sauti.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
  1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
  2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi10
  3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
  4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi10

Kumbuka msemo muhimu:

"Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa"

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | **Daraja 0** (Chekechea/Chini ya miaka mitano) **Daraja la Kwanza** (Miaka mitano hadi saba) **Daraja la Pili** (Miaka nane hadi kumi) | **Daraja la Tatu** (Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu) | **Daraja la Nne** (Miaka kumi na minne na zaidi) |
|---|---|---|---|
| **SOMO LA KUANZIA** | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi |
| **MFULULIZO WA A** | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| **MFULULIZO WA B** | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| **MFULULIZO WA C** | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

| | A1 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Hapo Mwanzo<br>Mada – Mungu aumba ulimwengu | A1 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Uumbaji<br>Mada – Hapo Mwanzo |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 1: 1-19***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 1: 1***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu aliumba ulimwengu na kila kitu kilichomo.<br>2. Mungu alimuumba, anamjua na anampenda kila mtu. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 1: 1-31***<br>**Mstari Muhimu:** ***Waebrania 1: 10; Isaya 45: 18***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu aliuumba ulimwengu.<br>2. Mungu ni mwenye nguvu zote.<br>3. Mungu alimuumba mtu kwa mfano wake. |
| **TOA UTANGULIZI** | Mwambie kila mwanafunzi aandike majibu ya maswali yafuatayo. Inaruhusiwa kukisia! Wanafunzi wanaweza kuwashirikisha jirani zao majibu.<br><br>1. Je, kuna nyota ngapi angani?<br>2. Je, kuna watu wangapi duniani?<br><br>Baada ya dakika chache, weka wazi majibu yafuatayo:<br>• Kwa mujibu wa Wakala wa anga la Ulaya (European Space Agency), ni vigumu kusema kwa usahihi idadi ya nyota. Inakadiriwa kuwa katika galaksi yetu ya Njia Nyeupe (Milky Way Galaxy kwa Kiingereza) pekee, kuna nyota milioni 100 elfu (laki moja). Pia kuna mamilioni ya nyota katika anga zingine! Ni nyota nyingi mno!<br>• Kwa sasa inakadiriwa kuwa, kuna watu takribani bilioni 7 duniani. | Jadili maswali yafuatayo kwa vikundi vidogo vya watu wawili wawili na baadaye yajadili kwenye darasa zima:<br><br>1. Je, ni lini mara ya mwisho ulifanya jambo la ubunifu?<br>2. Je, ulifurahia matokeo ya ubunifu huo? |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kabla ya kitu chochote kuwepo, Mungu alikuwepo.<br>2. Mungu aliumba ulimwengu kwa siku sita.<br>3. Siku ya kwanza Mungu aliumba nuru na akaitenga na giza; Siku ya pili Mungu aliumba anga na akalitenganisha na maji yaliyo chini. Siku ya tatu Mungu aliyakusanya maji na akapaita mahali pakavu, nchi. Nchi ikazalisha mimea. Siku ya nne Mungu aliweka mianga kwenye anga la mbingu: jua, mwezi na nyota; Siku ya tano Mungu aliumba viumbe wanaoishi majini na ndege; Siku ya sita Mungu alifanya wanyama.<br>4. Kisha Mungu alimuumba mtu kwa mfano wake, mwanamume na mwanamke, ili kuijaza na kutawala dunia na kila kiumbe.<br>5. Mungu aliwapa binadamu chakula na pia viumbe wake wote.<br>6. Mungu aliona kila alichokifanya, na tazama, ni chema sana! (***Mwanzo 1: 31)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – God creates the heavens and the earth. (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu aliumba ulimwengu kwa siku sita.<br>2. Siku ya kwanza Mungu aliumba nuru na akaitenga na giza; Siku ya pili Mungu aliumba anga na akalitenganisha na maji yaliyo chini. Siku ya tatu Mungu aliyakusanya maji na akapaita mahali pakavu, nchi. Nchi ikazalisha mimea. Siku ya nne Mungu aliweka mianga kwenye anga la mbingu: jua, mwezi na nyota; Siku ya tano Mungu aliumba viumbe wanaoishi majini na ndege; Siku ya sita Mungu alifanya wanyama.<br>3. Nguvu za Mungu zinashangaza: Aliumba ulimwengu kwa kutamka, na ilimchukua siku sita tu!<br>4. Mungu aliwaumba binadamu kwa mfano wake; Aliwaumba mwanamume na mwanamke.<br>5. Mungu alipoona kila kitu alichokifanya, tazama, ni chema sana. (***Mwanzo 1: 31)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – God creates the heavens and the earth. (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Kwenye vikundi vya watu wanne, tengeneza bango linaloonesha kila siku katika siku zile sita za uumbaji wa Mungu. | Umejifunza nini kuhusu tabia ya Mungu kwenye somo hili? Andika shairi fupi, mchezo (word puzzle) au aya kuelezea tabia ya Mungu. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mungu ni mwenye nguvu zote na aliumba kila kitu. Hata kama uumbaji wake ni mkubwa na wenye mambo mengi, Mungu alimuumba, Mungu anamjua na kumpenda kila mmoja wetu. Je, jambo hili linatakiwa liathiri vipi mutazamo wangu kumhusu Mungu na uumbaji wake? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mungu aliuumba ulimwengu wetu na alituumba pia. Jambo hili linatakiwa kuleta utofauti upi kwenye maisha yetu?<br>2. Soma ***Mwanzo 1: 26-27 & Isaya 45: 18***. Je, Mungu alikuwa na maono yapi kwa ajili ya binadamu? Je, jambo hili linaathiri vipi maisha yetu ya leo? |

| | **A1 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Pili – Hapo Mwanzo**<br>**Mada – Mungu amwumba mwanadamu** | **A1 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Pili – Uumbaji**<br>**Mada – Kukamilika** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 1: 20-31***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 1: 27***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu aliwaumba wanyama lakini binadamu akamuumba kwa namna ya tofauti.<br>2. Mungu alimuumba binadamu kwa mfano wake, ili awe kama yeye na atawale uumbaji.<br>3. Mungu aliwafanya watu ili wawe na mahusiano naye na pia wawe na mahusiano wao kwa wao.<br>4. Mungu alimpa binadamu majukumu. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 1: 27-31; 2: 1-9***<br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 1: 1-3***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alipumzika siku ya saba.<br>2. Mungu aliiumba Sabato kwa ajili ya mapumziko.<br>3. Mungu alimpa binadamu uhai.<br>4. Maisha ya Binadamu yana thamani ya pekee. |
| **TOA UTANGULIZI** | Cheza mchezo wa kuchagua wanyama (Animal Pictionary kwa Lugha ya Kiingereza). Gawa darasa katika makundi ya watu wanne. Wape kila kikundi karatasi na kalamu. Mtu mmoja katika kila kikundi atachora mnyama yeyote na watu wengine katika kikundi chake watasema mnyama aliyechorwa ni yupi. | Majadiliano ya kutembea (Walking debate kwa Lugha ya Kiingereza). Weka lebo ya maneno “Nakubali”, “Sikubali” na “Sina Uhakika” ili kuwa na ‘vituo’ vitatu pale darasani. Soma kauli zifuatazo na uwaambie wanafunzi/watoto waende wasimame kwenye kituo kinachoashiria mawazo yao kuhusu kauli hizo.<br>• Yale mawazo kuwa, Jumapili ni siku maalum, ni jambo lililopitwa na wakati.<br>• Jumapili ni siku nzuri ya kumalizia kazi za shuleni na kwenda sokoni.<br>• Michezo inatakiwa ikatazwe au isiwe halali siku za jumapili.<br>• Inakubalika kufanya utafiti wa kimatibabu kwa kuwatumia watoto walioko tumboni (kiinitete au embryo kwa Lugha ya Kiingereza).<br>• Wakristo hawatakiwi kushiriki vitani. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu aliwaumba wanyama wazuri ili kuzaana na kuogezeka.<br>2. Mungu aliwaumba binadamu kwa mfano wake, ili wawe kama yeye, wakawatawale samaki, ndege na wanyama.<br>3. Mungu aliwaumba watu. Alimuumba mwanamume na mwanamke.<br>4. Mungu aliwabariki wanadamu na akawapa kazi na majukumu maalum (aliwaambia wazae na waongezeke, wakaijaze nchi na kuitiisha, na kuwatawala viumbe wote wa Mungu).<br>5. Mungu alitoa vyanzo vya vyakula – kila tunachokihitaji kwa ajili ya kuiishi.<br>6. Mungu aliona kila alichokifanya. Akasema ni chema sana!<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – God creates the heavens and the earth. (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Hapo mwanzo, kabla ya kuwepo kwa kitu chochote, Mungu alikuwepo. Neno (Bwana Yesu) ni Mungu na alikuweko kwa Mungu hapo mwanzo. Aliumba kila kitu kilichoumbwa; wala pasipo yeye hakuna kilichoumbwa. Mungu ni muumbaji na Yeye ni Mungu wa kuanzisha vitu au Mungu wa mwanzo.<br>2. Mungu alimweka mtu katika Bustani ya Edeni.<br>3. Mungu pia aliweka miti miwili maalum katika Bustani ya Edeni; Mti wa Uzima, na Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya.<br>4. Mungu alipumzika siku ya saba na akaweka utaratibu wa siku maalum kwa ajili ya mapumziko kwa binadamu.<br>5. Mungu alimpulizia mtu pumzi ya uhai puani. Hii ilimfanya binadamu kuwa wa tofauti na wanyama. Maisha ya binadamu ni ya kipekee na yana thamani ya pekee.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – God creates the heavens and the earth. (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Jadili kwenye vikundi vidogo, kisha wanafunzi watoe majibu yao kwa watu wote:<br>Mungu aliwaumba watu kwa mfano wake wakatawale samaki, ndege na wanyama. Je, tunatakiwa kuwafanyia nini?<br><br>Mungu alituumba ili tuwe na mahusiano naye na watu wengine. Je, tunaweza kuonesha upendo wetu kwa Mungu na kwa watu wengine kwa njia zipi tukiwa 1) nyumbani 2) shuleni na 3) kanisani? | Jadili kwenye vikundi vidogo, kisha wanafunzi watoe majibu yao kwa watu wote:<br>Soma ***Kutoka 20: 8*** na ***Marko 2: 27***. Je, mistari hii ina maana gani katika maisha yetu siku ya leo?<br><br>Tumejifunza kuwa maisha ya binadamu ni ya thamani ya pekee. Je, jambo hili linaweza kuathiri vipi maamuzi kwenye masuala ya sayansi, tiba, sheria na utunzaji wa wazee? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mungu alituumba ili tuwe na mahusiano naye na watu wengine. Maisha yetu yatakuwa na tofauti gani kila siku tukitubu na kumwamini Mungu?<br>2. Mwombe Mungu ili atusaidie kutimiza wajibu wetu na tuoneshe tabia yake (kwa mfano upendo wake, wema, haki) juma hili katika familia, shule na katika vikundi vya kanisani. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tunawezaje au tunashindwaje kuiishi kwenye mapumziko ya Sabato kwenye maisha yetu leo? Je, mapumziko ya sabato ni muhimu? Kwanini?<br>2. Je, tutahakikisha vipi kuwa maisha yetu yanaonesha imani yetu kwamba maisha/uhai wa binadamu unatolewa na Mungu na una thamani ya pekee? |

| | A1 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Hapo Mwanzo<br>Mada – Mambo kuharibika | A1 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Uumbaji<br>Mada – Ujio wa Dhambi |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 2: 15-17; Mwanzo 3: 1-13***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 3: 3***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Adamu na Hawa hawakumtii Mungu.<br>2. Adamu na Hawa waliona aibu na walipata adhabu ya dhambi yao. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 2: 14-19; Mwanzo 3: 1-7***<br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 3: 23; Warumi 6: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alimwamuru mtu asile tunda katika mti wa ujuzi wa mema na mabaya<br>2. Nyoka alimdanganya Hawa na Adamu na Hawa akaasi amri ya Mungu.<br>3. Adamu na Hawa waliona aibu. |
| TOA UTANGULIZI | Waulize wanafunzi kama wana sheria shuleni kwao. Je, hizi sheria zina umuhimu gani? Je, nini kinaweza kutokea watu wakizipuuza sheria hizi? | Waambie wanafunzi wajadili yafuatayo wakiwa kwenye vikundi vya watu wawili wawili:<br>Majukumu waliyonayo shuleni/kazini/nyumbani.<br>Utaratibu au mwongozo wanaotakiwa kuufuata.<br>Je, nini kinaweza kutokea watu wakizipuuza sheria hizi au kutozitilia maanani? |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimweka mtu kwenye bustani ya Edeni na akampa kazi ya kuitunza. Mungu alimpa mtu kila kitu alichokihitaji, lakini kuna amri moja ambayo mtu alitakiwa kuitii. Hakuruhusiwa kula matunda ya ‘Mti wa ujuzi wa mema na mabaya’. Mungu alisema kuwa, akiyala, hakika atakufa.<br>2. Mtu akapewa kazi ya kuwapa majina wanyama na ndege.<br>3. Mungu akamuumba mwanamke ili amsaidie mwanamume kwenye majukumu yake. Kwenye ndoa, mwanamume na mwanamke wanaungana na kuwa na familia mpya na kushirikiana kama timu.<br>4. Nyoka mwenye hila ambaye ni adui wa Mungu, aliyekuja kwa kujificha, alileta mashaka kwenye ile amri ya Mungu. Aliwaambia Adamu na Hawa kuwa wasingekufa wakiivunja ile amri ya Mungu. Yule nyoka akamdanganya mwanamke naye akala tunda ambalo Mungu alikuwa amewaambia wasile. Akampa mwanamume naye akala pia.<br>5. Baada ya kufanya hayo, mwanamke na mwanamume wakakosa furaha. Wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo ili kujifunika na wakajificha kati ya miti ya bustani. Mungu akawaita na wakamwambia walichokuwa wamekifanya. Adamu alimlaumu Hawa naye Hawa alimlaumu nyoka.<br>6. Mungu akamlaani nyoka. Adamu na Hawa walipata adhabu ya dhambi yao. Walipata uchungu na iliwapasa kupambana na kufanya kazi kwa bidii. Maisha yakawa magumu na siku moja kifo kingewapata.<br>7. Mungu akawafanyia mavazi ya ngozi akawavika Adamu na Hawa. Akawafukuza bustani ya Edeni mbali na Mti wa Uzima.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Adam and Eve disobey Mungu and face the consequences. (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimpa Adamu kazi ya kuitunza bustani ya Edeni na kuwapa majina wanyama na ndege.<br>2. Mungu alisema mtu angeweza kula kutoka kwenye miti yote pale kwenye bustani isipokuwa kutoka kwenye mti mmoja; Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya. Mungu alisema matokeo ya kula kutoka kwenye mti huo ni kifo.<br>3. Mungu akamfanyia mwanamume msaidizi aitwaye mwanamke. Walipaswa kushirikiana. *Kwenye ndoa, mwanamume na mwanamke wanaungana na kuwa na familia mpya na kushirikiana kama timu.*<br>4. Yule nyoka mwenye hila alimdanganya Hawa naye akakosa kumtii Mungu, akala tunda alilokatazwa na akampa mwanamume naye akala pia. Mwanamume alimwasi Mungu kwa kula tunda. Adamu na Hawa wote wakapungukiwa na kile kiwango kikamilifu cha Mungu kwa kula tunda.<br>5. Adamu na Hawa walijua kuwa walikuwa wamekosa kumtii Mungu na wakaona haya. Hawakuwa na budi kupata matokeo ya uamuzi wao wa kutotii amri ya Mungu.<br>6. Walipata adhabu ya Mungu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Adam and Eve disobey Mungu and face the consequences. (I)** |
| REJELEA SOMO | Unganisha somo hili na ***Warumi 5: 12***. Tangu Adamu na Hawa walipomkosea Mungu, wote tumezaliwa wenye dhambi. Waulize wanafunzi wafikiri kuhusu mifano ya kutokumtii Mungu katika maisha yetu.<br>Je, jambo hili lina athari gani 1) kwetu na 2) kwa watu wengine? | Je, matokeo ya kutotii kwa Adamu na Hawa yalikuwa ni nini? Soma ***Warumi 5: 12-14*** na ***18-19***.<br>Je, kule kutotii kwa Adamu na Hawa kumetuathiri vipi kwenye maisha ya leo? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Tunapaswa kumwomba Mungu msamaha ili atusamehe na kutufanya upya. Kisha tuweza kuishi maisha ya kumpendeza na kutii amri zake. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Kama Wakristo, kwanini ni muhimu kumtii Mungu? Je, tunawezaje kumtii Mungu kwa vitendo na uhalisia katika maisha yetu leo? |

| | A1 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Uumbaji<br>Mada – Kufanya mambo kwa njia ya Mungu | A1 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Uumbaji<br>Mada – Matokeo ya Dhambi |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 4: 1-16***<br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 14: 6***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Habili alifuata njia ya Mungu, ila Kaini alifuata njia yake mwenyewe. Mungu aliikubali sadaka ya Habili ila aliikataa ile ya Kaini.<br>2. Kaini alimuua Habili. Mungu alimfukuza katika uso wa ardhi na kumfanya awe mtoro. Kaini akatoka mbele za uso wa Bwana.<br>3. Kuna njia moja tu ya kwenda kwa Mungu, na njia hiyo ni njia yake. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 3: 7-24***<br>**Mstari Muhimu:** ***1 Wakorintho15: 22; Warumi 6: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Adamu na Hawa walijaribu kujificha mbele za Mungu.<br>2. Mungu akamlaani yule nyoka mwenye hila.<br>3. Mungu akawaambia Adamu na Hawa kuwa watapata uchungu na ugumu kwa sababu ya dhambi yao.<br>4. Mungu akawafanyia Adamu na Hawa mavazi na kuwavika ili kuficha uchi wao.<br>5. Mungu akawafukuza Adamu na Hawa kutoka bustani ya Edeni. |
| **TOA UTANGULIZI** | Kitu gani kitatokea ukianza safari bila kuangalia ramani au mwelekeo? Je, umewahi kupuuzia maelekezo kisha ukapotea? Kaini hakufuata maelekezo ya Mungu na hatima yake akawa mtoro aliyepotea. | Waambie wanafunzi wafikiri kuhusu wakati ambapo hawakutii kwenye utoto wao wakiwa nyumbani au shuleni.<br>Je, jambo hili liliwapa hisia gani? |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Adamu na Hawa walikuwa na wana wawili. Habili alikuwa mchunga kondoo naye Kaini alikuwa mkulima ardhi.<br>2. Mungu aliikubali sadaka ya wanyama aliyoileta Habili: Wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. Mungu aliikataa sadaka ya kaini: Sehemu ya mazao yake. Kaini akaghadhabika sana na uso wake ukakunjamana.<br>3. Mungu alimuonya Kaini kuhusu dhambi na akamwambia umuhimu wa kufuata njia ya Mungu ambayo ni ya haki. Kaini hakuomba msamaha na pia hakumsikiliza Mungu.<br>4. Kaini akamwua Habili, ndugu yake. Mungu akamfukuza katika uso wa ardhi na akawa mtoro mbali, akatoka mbele za uso wa Bwana.<br>5. Habili alielewa kuwa, ilimpasa kumtoa mwana-kondoo kwa Mungu. Kaini hakumjia Mungu kwa njia Yake, na aliadhibiwa.<br>6. *Sadaka ya Habili ilikuwa ni mfano wa sadaka ambayo Bwana Yesu angeitoa pale msalabani*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Cain and Abel (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kule kutotii kwa Adamu na Hawa kulileta ufahamu wa mema na mabaya na wakajiona wako uchi. Wakaogopa na wakataka kujificha mbele za Mungu.<br>2. Mungu akawauliza Adamu na Hawa maswali. Alitaka wakiri makosa waliyokuwa wameyafanya. Lakini, kila mmoja alimlaumu mwingine. Adamu alimlaumu Hawa naye Hawa alimlaumu nyoka.<br>3. Adamu na Hawa walipata matokeo ya kutokutii kwao: walipata uchungu, kusumbuka kwenye maisha na walifukuzwa kutoka kwenye bustani ya Edeni mbali na uwepo wa Mungu.<br>4. *Nasi pia, tunapata madhara ya dhambi yao – kwa kuwa Adamu alifanya dhambi, tunahusishwa naye, na sote tunaona kifo.*<br>5. Mungu ni Mungu mwenye utoaji uliojaa neema. Aliwapa Adamu na Hawa mavazi ya ngozi ili kuficha uchi wao. ***Warumi 6: 23*** inatufundisha kuwa Mungu anatoa bure karama ya uzima wa milele katika Bwana Yesu Kristo ikiwa tutamkubali kama Mwokozi wetu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Adam and Eve disobey Mungu. (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Kwenye Mstari Muhimu, Yesu alisema Yeye ndiye njia pekee ya kwenda kwa Mungu. Je, watu wanajaribu kumpendeza Mungu kwa njia zipi nyingine?<br><br>Tengeneza alamisho ya kitabu/ kifaa cha kutia alama kwenye kitabu (bookmark kwa Kiingereza) au kadi nzuri na uandike vizuri ule Mstari muhimu. | Je, tumejifunza nini kuhusu tabia ya Mungu kwenye somo hili? Husianisha somo hili na ***Warumi 5: 12***. Kutoka wakati ule ambao Adamu na Hawa walikosa kutii, sote tumezaliwa kama wenye dhambi. Waambie wanafunzi wafikirie kuhusu mifano ya kutotii amri za Mungu katika maisha yetu. Jambo hili lina athari gani 1) kwetu na 2) kwa watu wengine? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kariri Mstari Muhimu.<br>2. Je, unamfuata Yesu ambaye ndiye njia pekee ya kwenda kwa Mungu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mwombe Mungu nguvu ya kumtii na umshukuru kwa utoaji uliojaa neema anaotukirimia tunapomkosea.<br>2. Tunapaswa kumwomba Mungu msamaha ili atusamehe na kutufanya wapya, tuweze kuishi maisha yanayompendeza na kufuata amri zake. |

| | A2 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Nuhu na Gharika<br>Mada – Kujenga Safina | A2 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Kaini na Habili<br>Mada – Kumwabudu Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 6: 5-22***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 6: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu ni mtakatifu. Ile hali ya dhambi ya watu inamuumiza au kuvunja moyo wa Mungu.<br>2. Mungu aliamua kumwokoa Nuhu. Alimwambia ajenge safina ili aokoke yeye pamoja na familia yake na kila aina ya ndege na wanyama wawili wawili.<br>3. Nuhu alifanya kama alivyoelekezwa na Mungu kikamilifu. Nuhu alimwamini na kumtii Mungu. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 4: 1-16***<br>**Mstari Muhimu:** ***Waebrania 11: 4***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Habili alimwendea Mungu kwa njia ambayo Mungu mwenyewe aliitaka. Mungu aliikubali sadaka ya Habili.<br>2. Kaini alimwendea Mungu kwa njia yake mwenyewe. Mungu akaikataa sadaka yake. |
| TOA UTANGULIZI | Waoneshe wanafunzi maelekezo ya kujenga kitu fulani au hatua za kupika chapati. Ongea nao kuhusu umuhimu wa kufuata maelekezo unapotengeneza au kuandaa kitu. Waeleze kuwa Mungu alimpa Nuhu maelekezo maalum ya kujenga safina. Nuhu alifuata kwa ukamilifu yale maelekezo ya Mungu. | Orodhesha hali au mazingira tofauti yanayohitaji tufuate maelekezo. Je, kitu gani kitatokea tunapoyapuuza? |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Watu wakawa waovu sana duniani. Mungu akahuzunika sana moyoni kwa ajili ya dhambi na uaasi wao.<br>2. Mungu akaamua kuwaangamiza watu wote na wanyama aliowaumba.<br>3. Nuhu alikuwa tofauti. Alimpendeza Mungu. Alikuwa tofauti sana na watu wengine kwa sababu alifanya jambo sahihi, na alimpenda na kumtii Mungu.<br>4. Mungu alimwambia Nuhu kuwa anakwenda kuwaangamiza watu wote na viumbe hai kwa gharika kwa sababu wameijaza dunia dhuluma.<br>5. Mungu akampa Nuhu maagizo maalum kuhusu maandalizi. Alimwambia Nuhu jinsi ya kutengeneza safina ili kumwokoa Nuhu, familia yake na viumbe hai wa kila aina wawili wawili.<br>6. Nuhu alikuwa na imani kwa Mungu na alifuata maagizo yote kama alivyoambiwa.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Noah and the Great Flood (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Adamu na Hawa walikuwa na wana wawili. Habili alikuwa mchunga kondoo na Kaini alikuwa mkulima wa mazao.<br>2. Mungu aliikubali sadaka ya wanyama ambayo Habili alimletea: wazaliwa wa kwanza wa wanyama wake. Mungu aliikataa sadaka ya Kaini: sehemu ya mazao yake. Kaini akagadhabika sana.<br>3. Mungu akamuonya Kaini kuhusu dhambi na umuhimu wa kufuata maagizo ya Mungu. Kaini hakuomba msamaha na hakumsikiliza Mungu.<br>4. Kaini akamwua Habili, ndugu yake. Mungu akamfukuza atoke katika uso wa ardhi, akawa mtoro mbali na uwepo wa Mungu.<br>5. Habili alijua kwamba anapaswa kumtolea Mungu mwanakondoo. Kaini hakwenda mbele za Mungu kwa unyofu, akaadhibiwa.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Cain and Abel (I)** |
| REJELEA SOMO | Rejea habari kwa kutumia chemsha bongo kutoka kwenye somo la leo kuhusu Nuhu, familia yake na maelekezo ambayo Mungu alimpa Nuhu. | Soma Mstari Muhimu, ***Waebrania 11: 4***. Je, mstari huu unaziwasilishaje tofauti za Kaini na Habili? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Nuhu alimwamini Mungu, akafanya sawasawa na maagizo yake. Je, tunawezaje kuwa na imani kwa Mungu? Je, unamwamini? Nuhu alimwamini Mungu na Mungu akamwokoa. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Tunajifunza nini kutoka kwenye maisha na tabia za Kaini na Habili?<br>2. Je, tunawezaje kuyatenda mambo tunayojifunza kutoka kwenye maisha ya Kaini na Habili katika maisha yetu leo? |

| | A2 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Nuhu na Gharika<br>Mada – Ndani ya Safina | A2 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Henoko na Nuhu<br>Mada – Kutembea na Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 7: 1-20***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 7: 5***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alitoa njia ya kumwokoa Nuhu na familia yake.<br>2. Nuhu alikuwa na imani kwa Mungu na akafanya kama Mungu alivyomwambia kwa ukamilifu. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 5: 21-33; Mwanzo 6: 1-15***<br>**Mstari Muhimu:** ***Waebrania11: 5***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Henoko na kitukuu wake Nuhu, walitembea katika ushirikiano wa karibu na Mungu.<br>2. Hawa watu wawili walikuwa watu wa kipekee kwa sababu ya mahusiano yao na Mungu. |
| TOA UTANGULIZI | Je, umewahi kuwa safarini pamoja na familia yako? Je, ulijiandaa vipi kwa ajili ya hiyo safari? | Kuwa na mahusiano na Mungu kutatufanya tuwe watu wa kipekee kwenye umati! Je, Wakristo wanatakiwa kuwa tofauti na watu wengine kwa namna gani? Orodhesha tofauti hizo. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimtahadharisha Nuhu kuwa baada ya siku 7 angeleta gharika.<br>2. Mungu alimwambia Nuhu awaingize wanyama kwenye safina ili waokolewe na gharika.<br>3. Siku ile, ambayo ilikuwa ni siku ya 17 ya mwezi wa pili, Nuhu akiwa na umri wa miaka 600 aliichukua familia yake na wanyama, kama alivyoagizwa na Mungu na kuwaingiza kwenye safina. Baada ya siku saba gharika ilianza kama Mungu alivyosema.<br>4. Mungu alifunga mlango wa safina baada ya Nuhu na familia yake na wanyama kuingia ndani. Mungu aliwahifadhi ndani ya safina. Nuhu, familia yake na wanyama waliokuwemo ndani ya safina ndio walionusurika na ile gharika ya hatari. Mvua ilinyesha kwa siku 40! Maji yakapanda juu zaidi ya futi 22 na yakafunika hata milima mirefu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Noah and the Great Flood (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Henoko aliishi miaka 365, akitembea katika ushirika wa karibu na Mungu.<br>2. Biblia inasema kuwa Henoko hakufa kama watu wengine. Mwisho wa maisha yake alitoweka, kwa sababu Mungu alimpeleka mbinguni.<br>3. Nuhu alikuwa kitukuu wa Henoko. Kama Henoko, Nuhu pia alitembea katika ushirika wa karibu na Mungu na alikuwa mtu mwema tofauti na watu waovu waliomzunguka.<br>4. Katika siku za Nuhu, ule uovu wa watu ulimhuzunisha Mungu. Mungu akaamua kuwaadhibu kwa gharika, lakini akamwokoa Nuhu.<br>5. Mungu akampa Nuhu maelekezo ya kutengeneza safina ili yeye na familia yake waokolewe na gharika.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Noah and the Great Flood (I)** |
| REJELEA SOMO | Kuwa mbunifu! Chora picha ya Nuhu, familia yake na wanyama wakiwa ndani ya safina inayoelea juu ya maji. Picha yako iwe na kichwa cha habari “Okolewa na Mungu” | Je, Henoko na Nuhu walikuwa ni watu wa namna gani?<br>Je, ni kitu gani kiliwafanya wawe wa tofauti na watu wengine? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Mungu alimpenda Nuhu na akatoa njia ya yeye kuwa tayari ili amwokoe kutoka kwenye ile gharika. Kwanza, Nuhu alipaswa kufuata maelekezo ya Mungu. Mungu anatusihi tujiandae kwa ajili ya hukumu. Anataka tumwamini Bwana Yesu Kristo aliyekufa msalabani kwa ajili yetu ili kutuokoa. Je, umemwamini? Je, uko tayari kuokoka? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Rejelea ile orodha ya tabia zinazotakiwa kuwafanya Wakristo wawe watu wa tofauti kwenye umati.<br>Fikiria kuhusu Henoko na Nuhu na mahusiano yao na Mungu. Mwombe Mungu akusaidie ili uweze kumwamini na utembee katika mapenzi yake juma hili. Unaweza kuchagua tabia moja ya Mkristo mwaminifu na umwombe Mungu akusaidie kukua katika eneo hili. |

| | A2 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Nuhu na Gharika<br>Mada – Okolewa na Safina | A2 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Nuhu na Gharika<br>Mada – Kumfanyia Mungu kazi |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 8: 1-22***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 8: 1***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alimkubuka Nuhu na familia yake na wanyama waliokuwa kwenye safina.<br>2. Nuhu alimshukuru Mungu kwa sababu alimhifadhi salama kwenye safina.<br>3. Mungu aliweka ahadi ya kutoangamiza tena kila kilicho hai. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 6: 14-22; Mwanzo 7: 1-24***<br>**Mstari Muhimu:** ***Waebrania 11: 7***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alimpa Nuhu maelekezo ya kina kuhusu ujenzi wa safina.<br>2. Nuhu alitii maagizo ya Mungu kikamilifu na akaokolewa. |
| TOA UTANGULIZI | 1. Orodhesha njia ambazo familia yako, marafiki na walimu wako wanakutunza.<br>2. Orodhesha njia zote ambazo Mungu anazitumia kututunza kila siku.<br>3. Wakumbushe watoto umuhimu wa kushukuru familia zetu, marafiki na walimu wetu kwa yote wanayotutendea. Jambo muhimu zaidi ni kuwa, inatupasa kumshukuru Mungu anayetuokoa tunapomwamini. | Jadili na wanafunzi kuhusu maelekezo ya usalama yanayotolewa kwenye ndege, meli au mabasi. Je watu wanayazingatia? Je, kwanini wanayazingatia? Je, kwanini hawayazingatii? Je, kwa nini ilikuwa muhimu sana kwa Nuhu kutii maelekezo yote ambayo Mungu alimpa? |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimkumbuka Nuhu, familia yake na wanyama waliokuwamo kwenye safina. Mungu akavumisha upepo juu ya nchi na maji yakaanza kupungua.<br>2. Baada ya siku 150 (jumla ya miezi mitano) safina ikatua juu ya mlima uitwao Ararati. Baada ya miezi miwili na nusu maji yakapungua zaidi na milima mingine ikaonekana.<br>3. Baada ya siku 40 Nuhu akafungua madirisha ya safina akamtoa kunguru, ambaye hakurejea. Kisha akamtoa njiwa. Njiwa hakupata mahali pakavu, basi akarudi ndani ya safina. Baada ya siku 7, Nuhu akamtoa tena njiwa nje ya safina. Wakati huu akarejea na jani la mzeituni. Hivyo, Nuhu akajua kuwa maji yamekaribia kuisha juu ya nchi. Baada ya siku 7, Nuhu akamtoa yule njiwa, naye hakurudi tena.<br>4. Hatimaye, miezi kumi na miwili na nusu baada ya gharika, nchi ikawa kavu tena!<br>5. Mungu akamwambia Nuhu atoke nje ya safina pamoja na familia yake na wanyama.<br>6. Nuhu alijawa na shukrani. Alijenga madhabahu na akamtolea Mungu dhabihu ya kuteketezwa.<br>7. Mungu alipendezwa na sadaka ya Nuhu. Akaahidi kuwa hataangamiza tena viumbe wote hai.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Noah and the Great Flood (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimpa Nuhu maelekezo ya kina juu ya ujenzi wa safina na jinsi ya kufanya maandalizi kwa sababu ya gharika ambayo alikuwa amekaribia kuileta.<br>2. Mungu alimtahadharisha Nuhu kuhusu gharika kwa maelezo machache.<br>3. Mungu aliahidi kumwokoa Nuhu, familia yake na wanyama.<br>4. Mungu alitoa maelezo ya kina jinsi ya kuwaokoa wanyama. Nuhu, familia yake na wanyama waliingia ndani ya safina na Mungu akafunga mlango.<br>5. Gharika ilidumu kwa siku 40 na kila kiumbe hai kilichokuwa nje ya safina kiliangamia katika ile mvua kubwa. Walionusurika ni Nuhu, familia yake na wanyama waliokuwemo ndani ya safina tu. Mungu aliwahifadhi, wakiwa ndani ya safina, walielea juu ya maji ya gharika.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Noah and the Great Flood (I)** |
| REJELEA SOMO | Tengeneza bango na uweke vitu ambavyo tunapaswa kumshukuru Mungu kwavyo, hususani wokovu. | Je, tunajifunza mambo gani kuhusu tabia ya Nuhu na Mungu katika habari hii? Orodhesha maneno ambayo unaweza kuyatumia kuelezea kila mmoja wao. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Mungu alimwokoa na kumlinda Nuhu. Nuhu alikuwa mwenye shukrani kwa Mungu. Mungu anaweza na yuko tayari kutuokoa na kutulinda. Tunapaswa kumshukuru na kumwamini. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Soma Mstari Muhimu.Je, tunawezaje kufuata mfano wa Nuhu kwenye maisha yetu?<br>2. Je, jambo hili linaweza kuwagusa vipi watu wanaotuzunguka? |

| | **A2 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Nne – Nuhu na Gharika**<br>**Mada – Nje ya Safina** | **A2 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Nne – Nuhu na Familia yake**<br>**Mada – Kumwabudu Mungu** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 9: 7-17***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 9: 15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu aliweka agano na Nuhu. Aliahidi kuwa hataangamiza tena viumbe wote hai duniani kwa maji ya gharika.<br>2. Mungu akaweka upinde wa mvua angani kama ishara ili kukumbuka ahadi yake. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 8: 1-22; Mwanzo 9: 11-16***<br>**Mstari Muhimu:** ***Waefeso 2: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alimkumbuka Nuhu, familia yake na wanyama waliokuwamo ndani ya safina.<br>2. Nuhu alishukuru na kumwabudu Mungu kabla ya jambo lolote mara tu alipotoka kwenye safina.<br>3. Mungu aliahidi kutoangamiza tena viumbe wote hai duniani kwa maji ya gharika. |
| **TOA UTANGULIZI** | Kwenye vikundi vya watu wawili wawili, jadili kuhusu ahadi tofauti ambazo watu huweka. Je, kila wakati watu wanatimiza ahadi zao? | Kwenye vikundi vya watu wawili wawili: jadili zawadi mbalimbali ambazo watu hutoa kama ishara ya shukrani. Je, kwanini watu wanatoa zawadi hizi?<br>Je, umewahi kutoa zawadi kama hii? Kwanini? |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu aliwaambia Nuhu na familia yake, zaeni mkaongezeke mkaijaze nchi.<br>2. Mungu aliweka ahadi maalum inayoitwa agano na Nuhu na wana wake na wanyama na viumbe hai wote juu ya nchi.<br>3. Mungu akaahidi hataangamiza tena dunia na viumbe wote hai kwa maji ya gharika.<br>4. Mungu akaweka upinde wa mvua mawinguni ili iwe kama kumbukumbu ya agano ambalo litadumu milele. Kamwe hatavunja ahadi yake.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Noah and the Great Flood (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimpa Nuhu maelekezo ya kina kuhusu ujenzi wa safina na kuhusu kujiandaa kwa ajili ya gharika ambayo alikuwa amekaribia kuileta<br>2. Mungu aliahidi kumwokoa Nuhu, familia yake na wanyama waliokuwemo ndani ya safina.<br>3. Gharika ikaja na kudumu kwa siku 40. Nuhu, familia yake na wanyama waliokuwemo ndani ya safina ndiyo walionusurika tu!<br>4. Gharika ikaisha na maji yakapungua taratibu. Safina ikatua juu ya mlima Ararati.<br>5. Baada ya siku 40, Nuhu akamtoa kunguru nje ya safina. Kunguru aliruka huku na kule hadi maji yalipokauka juu ya nchi. Kisha, akamtoa njiwa. Hakupata sehemu ya nchi kavu iliyokauka ya kutua hivyo basi akarudi kwenye safina. Baada ya siku 7, Nuhu akamtoa tena njiwa nje ya safina. Wakati huu njiwa alirudi kwenye safina akiwa na jani la mzeituni mdomoni mwake. Kwa mara nyingine, Nuhu akamtoa yule njiwa nje ya safina, mara hii hakurudi, nchi ilikuwa imekauka.<br>6. Mungu akamwambia Nuhu na familia yake, watoke nje ya safina na wakaongezeke na kuijaza nchi.<br>7. Jambo la kwanza ambalo Nuhu alilifanya mara tu alipotoka nje ya safina lilikuwa ni kumtolea Mungu dhabihu.<br>8. Mungu aliweka ahadi maalum inayoitwa agano na Nuhu na wana wake na wanyama na viumbe hai wote juu ya nchi.<br>9. Mungu akaahidi hataangamiza tena dunia na viumbe wote hai kwa maji ya gharika.<br>10. Mungu akaweka upinde wa mvua mawinguni ili iwe kama kumbukumbu ya agano ambalo litadumu milele. Kamwe hatavunja ahadi yake.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Noah and the Great Flood (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Kuwa mbunifu! Tengeneza bango la upinde wa mvua. Lipe kichwa, "Mungu anatimiza ahadi zake milele" | Jadili katika vikundi na mtoe majibu kwa pamoja:<br>Je, somo hili linatufundisha nini kuhusu kuabudu? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Ahadi ya Mungu kwa Nuhu ni ya milele. Mungu anatimiza ahadi zake siku zote! Je, jambo hili linapaswa kuleta mabadiliko yapi kwenye maisha yetu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Nuhu alikuwa mwenye shukrani kwa Mungu. Kwa vitendo, je, tunawezaje kuonesha shukrani zetu kwa Mungu? |

| | **A3 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Kwanza – Maisha ya Petro**<br>**Mada – Yesu amwita Petro** | **A3 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Kwanza – Maisha ya Petro**<br>**Mada – Wito Wake** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 4: 17-22***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 4: 19***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu anawaita watu wamfuate.<br>2. Kumfuata Yesu kunamaanisha kumwamini na kutubu na kuacha dhambi. | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 4:17-22; Yohana 1:35-42***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 4: 19***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Andrea na labda Yohana walikuwa wa kwanza kukutana na Yesu, baadaye wakawa wanafunzi wake.<br>2. Waligundua kuwa Yesu ndiye Masihi na Mwokozi. |
| **TOA UTANGULIZI** | Zungumza kuwa katika michezo au miradi mbalimbali unahitaji vikundi vya watu ambao watafanya kazi pamoja. Yesu alikuwa anaanza huduma yake na alihitaji watu ambao angewaandaa ili waendeleze kazi yake atakapokuwa ameondoka. | Zungumza jinsi ambavyo watu wanaweza kuwa mashabiki au wapenzi wa timu ya mpira wa miguu, waimbaji wa muziki na kadhalika.<br>Elezea kuwa tabia ya Yesu na maneno yake yaliwavutia sana watu kwake. Pia elezea kuwa, Yesu aliwaita watu maalum kuwa wanafunzi wake. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Ujumbe ambao Yesu aliuhubiri ***(Mathayo 4: 17)***<br>2. Yesu aliwaona Petro na Yohana wakitupa jarife baharini.<br>3. Yesu aliwaita wavuvi waliokuwa wanafanya kazi kwa bidii na kwa kushirikiana. Alijua kuwa wangeweza kufundishwa ili kufanya kazi yake.<br>4. Ule utii wao bila kusita kwa wito huo.<br>5. Yesu pia aliwaita Yakobo na Yohana, nao pia wakamtii mara moja. Hawa walikuwa wanafunzi wa kwanza.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha: Hakuna picha inayofaa habari hii kwenye tovuti ya FBI .** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yohana Mbatizaji alisema kuwa Yesu ni Mwanakondoo wa Mungu naye Andrea na rafiki yake walijua kuwa ni Masihi. ***(Yohana 1: 35, 41)***<br>2. Umuhimu wa Andrea kumtambulisha Petro kwa Yesu.<br>3. Hawakushangaa walipokutana na Yesu baadaye wakiwa wanavua samaki.Yesu aliwaita ili wamfuate nao walitii mara moja.<br>4. *Ule ushuhudiaji binafsi wa Andrea.*<br>5. *Ule umuhimu wa kumwona Kristo katika maisha na kuwaambia wengine kuhusu jambo hili.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha: Hakuna picha inayofaa habari hii kwenye tovuti ya FBI .** |
| **REJELEA SOMO** | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Je, kwanini Yesu aliwaita watu hawa?<br>2. Je, kutii wito wa Mungu kuna maanisha nini kwenye maisha ya leo?<br>3. Je, ni mambo gani ambayo yanafanya iwe vigumu kutii wito wa Mungu?<br>4. Je, Yesu aliwaahidi nini? ***(Angalia Mathayo 4: 19)*** | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Je, utajua vipi kwamba Mungu ana mpango kwa ajili ya maisha yako?<br>2. Je, Yesu alikuwa na mpango upi kwa ajili ya wanafunzi wake wa kwanza?<br>3. Je, faida za kujua mpango wa Mungu ni zipi?<br>4. Je, tunawezaje kujua mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha yetu, na tunapaswa kuitikia vipi? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Jadili maana ya toba kwa siku za leo.<br>2. Andika sala ya toba na uiweke kwenye kopo lililoandaliwa kwa ajili hiyo.<br>3. Tafiti kuhusu wito wa Wakristo wanaofahamika sana kwenye nyakati za leo kwa mfano David Livingstone. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Jadili jinsi gani tunaweza kushuhudia siku za leo.<br>2. Orodhesha majina ya Yesu. |

| | A3 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Maisha ya Petro<br>Mada – Samaki wengi wavuliwa | A3 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Maisha ya Petro<br>Mada – Changamoto yake |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 5: 1-11***<br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 3: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wanafunzi walijifunza kumtii Yesu.<br>2. Yesu ni mkuu na mwenye nguvu na anaweza kufanya miujiza ya ajabu.<br>3. Mungu anaweza kumtumia mtu yeyote akitubu. | **Neno la Biblia:** ***Mathayo: 14: 22-33***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 14: 33***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wanafunzi walijifunza kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, na anaweza kutuliza hofu zetu.<br>2. Kumwamini Yesu kunatuwezesha kushinda wakati wa dhoruba za maisha. |
| TOA UTANGULIZI | Zungumzia jinsi gani, kwenye mazingira ya shule kuna mitihani au majaribio mbalimbali ili kuangalia uelewa wa wanafunzi kuhusu masomo waliyofundishwa.<br>Yesu alikuwa anajaribu imani na utii wa wanafunzi kwenye tukio hili. | Elezea kuwa maisha yetu ni kama safari, inayoanza pale tunapozaliwa na inaendelea hadi tunapofariki.<br>Kuna wakati ambao maisha ni mazuri na kuna wakati ambao maisha ni magumu, wakati wa dhoruba. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yesu alikuwa anaongea na makutano akiwa kwenye mashua ya Petro.<br>2. Alipomaliza kuzungumza, akawaambia wakavue samaki tena. (Walikuwa wamevua usiku kucha bila kupata chochote na walikuwa wamechoka na wenye njaa).<br>3. Petro alifanya kama Yesu alivyoamuru na wakapata samaki wengi mno.<br>4. Petro alijua jinsi gani Yesu ni mkuu naye ni mwenye dhambi! ***(mstari wa 8)***<br>5. Wanafunzi waliacha kila kitu na kumfuata Yesu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jesus calls His first disciples (P)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yesu alifanya miujza mikuu na kisha akawaamuru wanafunzi wake wavuke bahari ya Galilaya.<br>2. Akaenda mlimani kuomba.<br>3. Wanafunzi walikuwa kwenye dhoruba.<br>4. Yesu alijua wanafunzi wako kwenye dhoruba na akawajia huku akiembea juu ya maji.<br>5. Petro akaomba kumwendea, naye akaweza kumwendea huku akitembea juu ya maji.<br>6. Akaanza kuzama,akapiga yowe huku akamwita Yesu na Yesu akamwokoa.<br>7. *Elezea umuhimu wa kumwamini Yesu.*<br>8. *Elezea jinsi gani, tunapomwamini Yesu, yeye anaweza kutusaidia kwenye dhoruba za maisha.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jesus walks on water (I)** |
| REJELEA SOMO | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Je, jibu la Simoni Petro kwenye ***mstari wa 5*** linamaanisha nini?<br>2. Je, tunajifunza nini kutoka kwa Petro kuhusu kule kutubu dhambi zake?<br>3. Jadili maana ya kutubu.<br>4. Je, tunawezaje “kuacha yote” kwa ajili ya Yesu? | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Je, maneno ya Yesu kwenye ***mstari wa 27*** yanawezaje kututia moyo?<br>2. Je, tunajifunza nini kutoka kwenye mfano wa Petro katika somo hili?<br>3. Je,tunajifunza nini tunapokumbana na dhoruba kwenye maisha yetu? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Orodhesha njia tatu ambazo unaweza kuzitumia kumtii Yesu kwenye juma lijalo<br>2. Mwombe Mkristo yeyote unayemfahamu akuambie kuhusu wakati ambao alijua kwa undani kuhusu msamaha wa Mungu. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Jadili kwa pamoja kuhusu ‘dhoruba’ kubwa ambayo umekumbana nayo katika maisha na ufikiri namna ambayo Yesu angekusaidia kwenye hali hiyo pale tunapomwamini.<br>2. Soma ***Isaya 43: 2.*** Je, mstari huu unamahusiano yapi na somo letu la Biblia la leo, ukizingatia wale wanaomfuata Yesu? |

| | **A3 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Tatu – Maisha ya Petro**<br>**Mada – Yesu amwokoa Petro** | **A3 – DARAJA LA NNE**<br>**Somo la Nne – Maisha ya Petro**<br>**Mada – Kukiri kwake** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 14: 22-33***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 14: 33***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu ni Mwana wa Mungu.<br>2. Kumtumaini Yesu kunatusaidia kushinda dhoruba za maisha na woga. | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 16: 23-28***<br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 10: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu ndiye “Kristo” au “Masihi”.<br>2. Jibu la Yesu kwa Petro linaweka msingi wa kanisa. |
| **TOA UTANGULIZI** | Ongelea kuhusu safari ya maisha. Elezea kuwa maisha ni kama safari inayonza pale tunapozaliwa na inaendelea hadi mwisho wa safari pale tunapofariki. | Ongelea kuhusu swali kubwa linalowasumbua watu wengi ambalo ni ‘Yesu ni nani hasa?’<br>Elezea kuwa katika zile nyakati za Yesu akiwa duniani, watu walitoa majibu tofauti kuelezea Yesu alikuwa nani, kisha Yesu akawauliza wanafunzi wake, je, wanadhani Yeye ni nani? |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yesu alikuwa amefanya muujiza mkuu na kisha akawaamuru wanafunzi wake kuvuka bahari ya Galilaya.<br>2. Akaenda mlimani kuomba.<br>3. Wanafunzi wakakumbwa na dhoruba.<br>4. Yesu alifahamu hilo na akawaendea huku akitembea juu ya maji.<br>5. Petro akaomba kumwendea na akafanya hivyo kwa kutembea juu ya maji.<br>6. Akaanza kuzama, akapiga yowe na kumwita Yesu naye Yesu akamwokoa.<br>7. *Elezea umuhimu wa kuwa na imani kwa Yesu.*<br>8. *Elezea jinsi gani Yesu anaweza kutusaidia katika dhoruba za maisha tunapomwamini.*<br>9. *Fikiri kuhusu umuhimu wa kumwamini Yesu katika wakati mgumu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jesus walks on the water (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yesu alikuwa upande wa kaskazini wa eneo alilokuwa amelitembelea (angalia ramani katika funzo)<br>2. Yesu akauliza, Je, “watu wanasema Mwana wa Adamu ni nani? Kuwa makini kuhusu majibu manne yatakayotolewa.<br>3. Kisha akauliza , “nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Angalia jibu la Petro la haraka.<br>4. Kisha akaelezea kuwa wote wanaoamini kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu aliye hai wanatengeneza Kanisa. Kanisa sio jengo bali ni kundi la watu wanaoamini.<br>5. Kisha Yesu akawaeleza kuwa ataenda kufa na baadaye atafufuka.<br>6. Petro akasema jambo hilo kamwe halitatokea. Angalia jibu ambalo Yesu alimpa Petro.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Hakuna picha inayofaa habari hii kwenye tovuti ya FBI .** |
| **REJELEA SOMO** | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Je, Yesu anawezaje kutusaidia kushinda hofu zetu?<br>2. Taja baadhi ya changamoto au matatizo ya kawaida ambayo vijana wanakumbana nayo.<br>3. Je, somo hili linawezaje kusaidia? | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Je, tunawezaje kuwa na uhakika kwamba sisi ni wa Yesu?<br>2. Je, tunawezaje kuwa sehemu ya Kanisa?<br>3. Je, ni mambo gani mazuri ambayo yanahusu kuwa sehemu ya kanisa? |
| **LIISHI SOMO** | 1. Tengeneza ukuta wa maonyesho (display wall kwenye Lugha ya Kiingereza) na uandike kwenye vikaratasi matatizo kisha uyagongelee msalabani.<br>2. Chora upinde wa mvua kisha uandike ahadi moja ya Biblia juu yake. | 1. Andika sala binafsi ya kumshukuru Mungu kwa ajili ya Kanisa lako.<br>2. Fikiri kuhusu mtu mmoja ambaye unaweza kumshirikisha Habari Njema za Yesu. |

| | A3 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Maisha ya Petro<br>Mada – Yesu ni nani? | A3 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Maisha ya Petro<br>Mada – Mlimani |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 16: 13-23***<br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 10: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Tunapaswa kushuhudia kuhusu Yesu ambaye ni Mwana wa Mungu.<br>2. Yesu ni Kichwa cha Kanisa. | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 17: 1-13***<br>**Mstari Muhimu:** ***2 Petro 1: 16-18***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu kama Mwana wa Mungu ni wa kipekee.<br>2. Yesu ni mkuu zaidi ya Musa au Elia. |
| TOA UTANGULIZI | Zungumza kuhusu watu maarufu na uelezee sababu za umaarufu wao. Yesu alikuwa amepata umaarufu ila watu wengi bado hawakujua yeye kwa hakika alikuwa ni nani. | Zungumza kuhusu matukio ya kusisimua ambayo wanafunzi kamwe hawawezi kusahau. Elezea kuwa, wale wanafunzi watatu kamwe wasingesahau lile tukio la kumwona Yesu akiwa kwenye utukufu wake pale mlimani. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yesu akauliza, Je, “watu husema Mwana wa Adamu ni nani? *Kuwa makini kuhusu majibu manne yatakayotolewa.*<br>2. Kisha akauliza, “nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Angalia jibu la Petro la haraka. *Elezea umuhimu wa ukiri wa Petro*<br>3. Kisha akaelezea kuwa wote wanaoamini kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu aliye hai wanatengeneza Kanisa. *Kanisa sio jengo bali ni kundi la watu wanaoamini.*<br>4. Kisha Yesu akawaeleza kuwa ataenda kufa na baadaye atafufuka.<br>5. Petro akasema jambo hilo kamwe halitatokea. Angalia jibu ambalo Yesu alimpa Petro.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha: Hakuna picha inayofaa habari hii kwenye tovuti ya FBI .** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yesu aliwachagua wanafunzi watatu ili wawe naye pale mlimani.<br>2. Alibadilika sura akawa katika utukufu na ukuu wake wote akiwa pamoja na Musa na Eliya.<br>3. Petro akataka waendelee kukaa na wajenge vibanda vitatu kwa ajili yao.Mungu akaongea kutoka mbinguni na kuwakumbusha kuwa Yesu ni mkuu sana kuliko mtu yeyote.<br>4. Wanafunzi wakaogopa lakini Yesu akawafariji na kuelezea kilichokuwa kimetokea.<br>5. *Elezea upekee wa Yesu na jinsi gani alivyo wa ajabu.*<br>6. *Fikiri kuhusu umuhimu wa kumpa nafasi ya kwanza kwenye maisha yetu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jesus is transfigured (I)** |
| REJELEA SOMO | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Je, kwanini maneno ya Petro (kwenye ***mstari wa 22***) hayakuwa sahihi?<br>2. Je, Kanisa letu linawezaje kutusaidia ili kumtumikia Mungu vyema zaidi?<br>3. Je, tunawezaje kuwa mashahidi bora, kuwaambia wengine kuwa Yesu ni nani hasa? | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Je, kwanini ilikuwa muhimu Petro kushuhudia tukio la kubadilika kwa Yesu?<br>2. Je, unafikiri wanafunzi walijifunza nini kuhusu hili tukio?<br>3. Je, tunawezaje kumpa Yesu nafasi ya kwanza kwenye maisha yetu? |
| LIISHI SOMO | 1. Tengeneza ukuta wa maonyesho (wall display kwa kiingereza) kwa kuchora mwonekano wa kanisa na uandike ndani ya mchoro huo faida za kuwa kama familia kanisani.<br>2. Kwenye kikaratasi andika jina la mtu ambaye ungependa kumshuhudia na kisha umwombee kila siku. | 1. Orodhesha vitu ambavyo vinatuzuia na kusababisha tushindwe kumpa Yesu nafasi ya kwanza katika maisha yetu.<br>2. ***Mstari wa 5*** unasema “Msikieni.” Panga muda juma hili ili usikie kile ambacho Mungu anakuambia. |

| | **A4 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Kwanza – Maisha ya Petro**<br>**Mada – Mfano wa Upendo** | **A4 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Kwanza – Maisha ya Petro**<br>**Mada – Masomo ya Unyenyekevu** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 13: 1-17***<br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 13: 15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikuwa Mtumishi wa kweli<br>2. Nasi pia tunapaswa kuwatumikia wengine. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 13: 1-17***<br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 13: 15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikuwa mtumishi mnyenyekevu, mwenye utii kwa mapenzi ya Mungu.<br>2. Unyenyekevu ni shina la utumishi katika Ukristo. |
| **TOA UTANGULIZI** | Nchi amabapo Yesu aliishi ilikuwa kavu na yenye joto kali. (Linganisha na nchi wanayoishi wanafunzi). Watu walikuwa wanatembea kwenye barabara zenye vumbi na walipofika kwenye nyumba, mwenye nyumba alihakikisha kuwa miguu yao imetawadhwa kabla ya chakula.<br>(Hebu fikiria desturi zilizopo katika nchi hii unapoingia kwenye nyumba) | Mara kwa mara, Bwana Yesu alielezea mambo ya muhimu kuhusu maisha ya Ukristo kwa kutumia mifano. Katika tukio hili aliamua kuweka kwenye vitendo mafundisho yake na jambo hili limeitwa "mfano katika vitendo". |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Ilikuwa ni siku moja kabla ya Yesu kusulubiwa, na alikuwa anapata chakula cha mwisho na wanafunzi wake.<br>2. Hakuna aliyejisumbua kufuata desturi za kawaida na kuwatawadha miguu yao. Yesu akajiandaa kufanya hivyo ***(Mistari ya 4 -5)***.<br>3. Petro akasema kuwa hataki Yesu amtawadhe miguu.<br>4. Yesu akaelezea kuwa ilimpasa kufanya hivyo, vinginevyo Petro asingekuwa na ushirika naye. ***(Mstari wa 8)***<br>5. Yesu alitumia kitendo cha kuwatawadha miguu ili kuonesha kuwa sote tu wachafu kwa ajili ya dhambi na tunahitaji kuoshwa na kutakaswa kutoka kwenye dhambi, na ni Yesu peke yake anaweza kufanya hilo kwa sababu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu.<br>6. Yesu pia alikuwa anatuonesha kuwa tunapaswa kujiandaa kufanya kazi za hali ya chini kwa ajili ya wengine.<br>7. *Elezea umuhimu wa kutawadhana miguu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jesus washes the disciples feet (P)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Yesu alikuwa anasherehekea Pasaka pamoja na wanafunzi wake. Sherehe hii ilikuwa ili kukumbuka yote yaliyotendeka wana wa Israeli walipotoka Misri.<br>2. Ilikuwa ni wakati huu wa chakula ambapo Yesu aliweka kwenye vitendo mafundisho mawili ya muhimu.<br>3. Kwanza, alichukua nafasi ya mtumwa na akawatawadha miguu ili kuonesha kuwa alikuwa tayari kufanya hata kazi za hali ya chini na kuwaonesha mfano mzuri. (Angalia Mstari Muhimu)<br>4. Alikuwa anawaonesha kuwa sote tunapaswa kutakaswa dhambi zetu. Hapa anatumia mfano wa kuoga, ***(mstari wa 10)***. Ila tunahitaji kutawadha miguu yetu kila siku tunapokuwa Wakristo kwani kila wakati tunatenda dhambi na tunahitaji msamaha.<br>5. Tazama jibu ambalo Yesu alimpa Petro ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa jambo hili.<br>6. Pili, akachukua mkate na divai na kuelezea kuwa mkate unawakilisha mwili wake kusulubiwa na divai iliwakilisha damu yake kumwagika pale msalabani. ***(Tazama Luka 22: 19 & 20)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jesus washes the disciples feet (P)** |
| **REJELEA SOMO** | 1. Jadili kuhusu njia halisi ambazo Wakristo wanaweza kuzitumia ili kuhudumiana kwenye juma lijalo.<br>2. Fikiri kuhusu njia halisi ambayo unaweza kuitumia kuhudumia kikundi ambacho sio sehemu ya kanisa lako mwaka ujao. | 1. Jadili njia ambazo tunaweza kuzitumia kuweka unyenyekevu kwenye vitendo katika maisha ya leo.<br>2. Fikiri kuhusu njia halisi ambayo tunaweza kuitumia kumpa Mungu nafasi ya kwanza kwenye maisha yetu.<br>3. Tafiti maisha ya Mkristo anayejulikana vyema kwa unyenyekevu katika utumishi wake. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, Yesu aliwatumikiaje wengine alipokuwa hapa duniani?<br>2. Yesu pia alikuwa anafundisha kuwa hata tunapokuwa Wakristo bado tunatenda dhambi na kila siku tunahitaji kutakaswa naye na kusamehewa dhambi. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, Petro alijifunza nini kutoka kwenye hili tukio?<br>2. Je, kuoshwa dhambi zetu kunamaanisha nini? Je, inatutupasa kufanya nini ili kuendelea kuwa karibu na Bwana na kufuata mapenzi yake kwa ajili ya maisha yetu? |

| | A4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Maisha ya Petro<br>Mada – Amkana Bwana Wake | A4 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Maisha ya Petro<br>Mada – Masomo ya Uaminifu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 22: 31-34, 54-62***<br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 22: 31-32***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ni vigumu kusema kuwa sisi ni wa Yesu.<br>2. Tunapaswa kusema ukweli kila wakati. | **Neno la Biblia:** ***Luka 22: 31-34, 39-62***<br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 22: 31-32***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Inatupasa kujiepusha na kule kujiamini bali tunapaswa kumwamini Yesu.<br>2. Tunapaswa kutubu dhambi zetu kwa kumaanisha kama Petro alivyofanya. |
| **TOA UTANGULIZI** | Fikiri kuhusu hali ambazo wanafunzi wanashawishika kusema uongo au kutokusema ukweli kwa ukamilifu. Chunguza kwanini wakati mwingine tunapata hofu sana kusema ukweli.<br>Eleza kuwa Petro alijikuta katika hali ya namna hiyo. | Petro alijidai kuwa asingemwacha Yesu na alikuwa tayari kwenda gerezani au hata kufa kwa ajili ya Yesu. ***(Luka 22: 33)*** Tunajua kuwa kiburi hutangulia uangamivu ***(Mithali 16: 18)*** Kwa Petro, kiburi chake kilitangulia kuanguka kwake kubaya. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Petro aliufuata msafara uliomkamata Yesu hadi kwenye nyumba ya Kuhani Mkuu.<br>2. Alikaa na baadhi ya watu wengine pale barazani mwa nyumba.<br>3. Baadhi ya watu walimuuliza kama alikuwa rafiki na mfuasi wa Yesu na mara tatu Petro alimkana Yesu na kuwaambia uongo.<br>4. Yesu akamtazama Petro, jogoo akawika na kisha Petro akagundua alichokuwa amekifanya. Akatoka nje na kulia kwa majonzi. Alikuwa amemwacha Yesu wakati ambapo Yesu alimhitaji zaidi. Alikuwa mwoga badala ya kuwa jasiri.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Peter denies Jesus (P & I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Lazima Petro alikuwa amechanganyikiwa! Alijua kile ambacho Yesu alikuwa amesema kuhusu kumkana. ***(Luka 22: 34)*** Alidhani alikuwa jasiri na angeweza kuwa na Yesu.<br>2. Wakati huu wa maswali ulipofika, Petro aliogopa sana kusema ukweli. Kwa kweli alimkana Yesu mara tatu kama Yesu alivyokuwa amesema.<br>3. *Fikiri jinsi gani Petro alijihisi kwa kumkana Yesu.*<br>4. *Jadili hali ya jaribu la Petro.*<br>5. *Pia, jadili umuhimu wa kuwa makina sehemu tunazoenda, watu tunaohusiana nao na pia jinsi tunavyofikiri.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Peter denies Jesus (P & I)** |
| **REJELEA SOMO** | 1. Orodhesha sababu zinazotufanya tushindwe kuwa watu wa Yesu na kisha uandike kweli / ahadi moja ya Biblia kuhusu sababu hizi.<br>2. Petro alikuwa amemkana Yesu, je, angesamehewa?<br>3. Tafuta namna ambayo Daudi alitubu ile dhambi aliyoifanya na Bethsheba ***(2 Samweli 11)*** kwenye ***Zaburi 51*** na akarejeshwa. | 1. Orodhesha sifa ambazo inatupasa kuangalia tunapotafuta marafiki wema.<br>2. Taja njia moja ambayo utaitumia juma hili kuonesha uaminifu wako kwa Yesu.<br>3. Fikiria kuhusu jambo ambalo Yesu alimaanisha alipomtahadharisha Petro kuhusu jambo ambalo lingetokea. ***(Luka 22: 32)*** |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, kwanini wakati mwingine inakuwa vigumu kwa Wakristo kusema kuwa wao ni wa Yesu?<br>2. Je, ni kitu gani kinatuzuia kuusema ukweli? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, tunawezaje kuonesha kuwa tuna masikitiko makubwa kwa ajili ya dhambi zetu?<br>2. Je, tutawezaje kuamua aina ya marafiki wa kuwa nao kila wakati? |

| | A4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Maisha ya Petro<br>Mada – Bwana Yesu afa | A4 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Maisha ya Petro<br>Mada – Masomo katika Huzuni na Furaha |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Marko 15: 22-40***<br>**Mstari Muhimu:** ***Wagalatia 2: 20***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikuwa mkamilifu na bila dhambi yeyote.<br>2. Tunapaswa kuwa na shukrani kwa ajili ya kifo cha Yesu pale msalabani. | **Neno la Biblia:** ***Luka 24: 1-12 & 33-49***<br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 24: 46-47***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alibeba adhabu ya dhambi zetu ili tuweze kuokolewa.<br>2. Yesu anatoa msamaha na uzima wa milele. |
| TOA UTANGULIZI | Jadili, je, wanafunzi wangefanya nini kama wamemkosea mtu kama vile Petro?<br>Fikiria kuhusu jambo ambalo Petro labda alijaribu kufanya lakini labda halikuwezeana. | Elezea kuwa hatujui kwa uhakika mambo ambayo Petro alikuwa anayafanya Yesu alipokuwa msalabani, lakini tunajua kuwa, kwenye Jumapili ya pasaka, Petro aliendа kaburini asubuhi na Biblia inasema kuwa alikutana na Yesu siku ile. ***(Tazama mstari 34)*** |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Elezea jinsi ambavyo Yesu alipelekwa nje ya mji ili kusulibiwa.<br>2. Elezea alivyotendewa, na jinsi alivyotukanwa na kudhihakiwa na watu waliokuwa wamemzunguka.<br>3. Fananua kule kuwa na giza la masaa matatu kulikuwa ni muujiza ambao unatusaidia kuelewa kuwa Mungu hakuweza kumwangalia Mwanaye ambaye alikuwa anaadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu.<br>4. Katika kipindi hiki Yesu alibeba adhabu ya dhambi zetu.<br>5. Elezea kitu kilichotokea kwa Yesu pale alipokufa. ***(Mistari ya 38-39)***<br>6. Elezea maneno ya yule akida aliyekuwa amesimama pembeni ya msalaba.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jesus is crucified and dies (P & I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Elezea jinsi ambavyo wanawake walienda kaburini asubuhi ya siku ya Pasaka.<br>2. Fafanua walikuta na nini na ujumbe waliopewa.<br>3. Eleza jambo ambalo Petro alilifanya alipopata habari hizo. (mstari wa 12)<br>4. Jadili kwanini watu wengine hawakuamini kuwa Yesu alikuwa amefufuka.<br>5. Elezea kilichotokea Yesu alipowatokea.<br>6. Petro na rafiki zake walikuwa na furaha ya ajabu walipomwona Bwana aliyekuwa amefufuka.<br>7. Je, Yesu aliyaelezea mateso yake kwa namna gani? ***(Mistari ya 45-47)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jesus is alive and risen from the dead (I &P)** |
| REJELEA SOMO | 1. Fikiria kuhusu kifo cha Yesu pale msalabani, maana ya Mstari Muhimu, na ule ukweli kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya kila mmoja wetu.<br>2. Jadili kuhusu faida za kifo cha Yesu pale msalabani. Fikiria kuhusu sehemu ambayo unaweza kuuweka msalaba kama ukumbusho wa ile sadaka ya Yesu. | 1. Jadili njia ambazo tunaweza kuzitumia kuonesha kuwa tunasikitika kwa ajili ya dhambi zetu.<br>2. Tunga maneno ya wimbo kusherekea ushindi wa Yesu juu ya kifo, na pia kufufuka kwake. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, unafikiri ni kwanini Yesu alikufa msalabani?<br>2. Je, tunawezaje kuonesha kuwa tunashukuru kwa ajili ya kifo cha Yesu pale msalabani? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, tunapataje uhakika kwamba Yesu yu hai?<br>2. Kuwa na uzima wa milele kunamaanisha nini?<br>3. Je, tunawezaje kujua kwamba tumesamehewa kwa hakika? |

| | A4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Maisha ya Petro<br>Mada – “Je, Wanipenda?” | A4 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Maisha ya Petro<br>Mada – Masomo ya Upendo |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 21: 1-17***<br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 21: 17***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Hata tunapomkosea Yesu kama Petro, bado tunaweza kusamehewa.<br>2. Yesu anataka tuwafundishe na kuwatunza wengine kama vile mchunga kondoo anavyowatunza kondoo wake. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 21: 1-20***<br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 21: 15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu yupo tayari kutupa mwanzo mpya.<br>2. Pamoja na udhaifu wetu, Yesu anatupenda sana. |
| TOA UTANGULIZI | Petro anajaribu kuanza tena maisha baada ya kifo cha Yesu. Anarudi mji alikotokea na kwa kazi aliyokuwa anaifanya. Anaenda kuvua samaki Bahari ya Galilaya. | Bwana Yesu anathibitisha kuwa yu hai, kwa kuwatokea mitume mara kadhaa baada ya kufufuka katika wafu.<br>***(1 Wakorintho 15: 3-8)*** |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wanafunzi walikuwa wamevua samaki usiku kucha bila kupata kitu chochote. Walikuwa wanarudi ufukweni wakiwa wamechoka, wanye njaa na wamevunjika moyo.<br>2. Bwana Yesu anawaita akiwa ufukweni lakini hawakumtambua. Anawauliza kama wana samaki.<br>3. Wanatii maelekezo yake na kutupa nyavu upande mwingine wa mashua na kisha wanapata samaki wengi mno.<br>4. Yohana anatambua kuwa mtu yule ni Yesu na inawezekana kuwa Petro aliogelea ili kumwendea.<br>5. Yesu anawaalika wote ili kupata kifungua kinywa na kisha anamuuliza Petro kama anampenda.<br>6. Petro anajibu kuwa anampenda na Yesu anampa kazi mpya ya kuwalisha wafuasi wake (kondoo).<br>7. *Jadili kwanini Yesu alimuuliza Petro swali lilelile mara tatu.*<br>8. *Fikiria namna ambayo Yesu alikuwa amemsamehe Petro kiasi cha kumpa kazi muhimu kama hii.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jesus appears to Disciples in Galilee and Jesus questions Peter (P)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Moja ya kujidhihirisha kwake baada ya kufufuka ni pale ambapo Yesu anawatokea wanafunzi wake saba wakiwa wanakuvua samaki kwenye Bahari ya Galilaya.<br>2. Aliwathibitishia yeye ni nani kwa kuwapa samaki wengi mno.<br>3. Wanafunzi wakapata kifungua kinywa pamoja na Bwana pale ufukweni.<br>4. Yesu alitaka kujua kama Petro alikuwa ametubu makosa aliyokuwa amemfanyia katika masaa ya mwisho ya uhai wake.<br>5. Mara tatu, Petro anaonesha upendo wake kwa Bwana mbele ya wengine.<br>6. Sasa Petro atakuwa mchunga kondoo ambaye atachunga wafuasi wa Bwana kwenye Kanisa jipya. Alikuwa anapewa fursa ya pili ya kumtumikia Bwana.<br>7. *Jadili, namna ambavyo Mungu anatupenda sana bila kujali udhaifu wetu na anataka tumpende pia.*<br>8. *Wakumbushe wanafunzi kuwa Mungu kamwe hawezi kutuacha ingawa mara nyingi tunamkosea.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Jesus appears to Disciples in Galilee and Jesus questions Peter (P)** |
| REJELEA SOMO | 1. Jadili njia halisi ya kutenga muda na kumsikiliza Yesu juma hili.<br>2. Tafiti kuhusu Mkristo maarufu ambaye alijifunza namna ya kumsikiliza Yesu na kisha kufanya mapenzi yake. | 1. Jadili jinsi gani upendo wa Mungu na msamaha wake unatutia moyo.<br>2. Tafiti kuhusu Mkristo maarufu ambaye Yesu alimpa mwanzo mpya. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Fikiria jinsi gani ilivyo muhimu kuonesha upendo wetu kwa Bwana kwa yote aliyotutendea.<br>2. Tambua kuwa Bwana yupo tayari kutupa fursa zaidi ya moja na kutusamehe tunapomkosea ikiwa tutaonesha toba ya kumaanisha. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, tunawezaje kuonesha kuwa tuna shukrani kwa ajili ya upendo wa Mungu kwetu sisi?<br>2. Kwa matendo yetu, je, tunawezaje kuthibitisha upendo wa Mungu kwetu? |

| | **A5 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Kwanza – Maisha ya Petro**<br>**Mada – Petro Ahubiri** | **A5 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la – Maisha ya Petro**<br>**Mada – Pentekoste** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 2: 1-43***<br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 1: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wafuasi wa Yesu walipewa Roho Mtakatifu kama zawadi.<br>2. Ujumbe au mafundisho ya wanafunzi ulikuwa; tunapaswa kutubu na kupokea msamaha wa Mungu. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 2: 1-42***<br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 2: 38***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Pentekoste ni sherehe ya Kiyahudi inayosherekewa siku tano baada ya Pasaka.<br>2. Baada ya mahubiri ya Petro, Kanisa likazaliwa. |
| **TOA UTANGULIZI** | Fikiria kuhusu hisia za wanafunzi ikiwa kuna mabadiliko makubwa katika maisha yao. Mabadiliko haya yanaweza kuwa shule mpya, nyumba au makazi mapya au mabadiliko katika familia.<br>Elezea kulikuwa na mabadiliko makubwa yanakuja kutokea kwa wanafunzi baada ya Yesu kurudi mbinguni na walipaswa kuendeleza kazi yake. | Fikiria kuhusu umuhimu wa siku za kuzaliwa, maadhimisho ya miaka (anniversaries kwa Lugha ya Kiingereza) na sherehe za kidini kwa kila familia. Fikiria kuhusu siku/tarehe muhimu katika miezi ijayo.<br>Taifa la Wayahudi walisherehekea Pentekoste ambayo ilikuwa ni siku hamsini baada ya Pasaka walipotoka Misri na Musa alipopokea Amri Kumi akiwa kwenye Mlima Sinai. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Wanafunzi walikuwa wanangojea ujio wa Roho Mtakatifu ambaye Yesu alikuwa amewaahidi. ***(Matendo 1: 8)***<br>2. Katika siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu alikuja kama ilivyoelezewa kwenye ***mistari ya 2-3***<br>3. Wanafunzi wakaanza kunena kwa lugha nyingine na watu waliokuwa wamekuja Yerusalemu kwa ajili ya sherehe maalum kutoka kwenye mataifa mbalimbali waliweza kuwaelewa.<br>4. Wengine walidhani kuwa wanafunzi walikuwa wamelewa.<br>5. Petro akasimama na kuwaelezea watu kitu kilichokuwa kimetokea. Anawaambia kuwa unabii wa Yoeli umetimia na Roho Mtakatifu amekuja. ***(Yoeli 2:28-32).***<br>6. Kwa ujasiri, Petro anawaambia kuwa walimuua Yesu lakini Mungu amemfufua katika wafu.<br>7. Walipoyasikia hayo walifadhaika na wakauliza wanatakiwa kufanya nini.<br>8. Petro anawaambia watubu na kubatizwa, siku hiyo watu elfu tatu wakaamini na kuwa wafusi wa Yesu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI –The Day of Pentecost (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Ahadi ya Bwana Yesu ilitimia pale wanafunzi walipompokea Roho Mtakatifu katika namna ya ajabu siku ile ya Pentekoste.<br>2. Elezea kilichotokea Roho Mtakatifu alipokuja.<br>3. Petro alisema kuwa taifa la Wayahudi walikuwa wamemwua Yesu lakini Mungu alimfufua na kumpeleka mbinguni na sasa alikuwa amemtuma Roho Mtakatifu.<br>4. Watu wote walioamini siku ile wakawa waumini wa kwanza wa Kanisa.Kanisa lilianza siku ile na linaendelea hata leo.<br>*5. Jadili, kitu gani haswa kilitokea kwa wale walioamini.* ***(angalia mistari ya 38-39).***<br>6. *Tazama walichokifanya ili kuonesha kuwa maisha yao yalikuwa yamebadilika.* ***(angalia mstari wa 42)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI –The Day of Pentecost (I)** |
| **REJELEA SOMO** | 1. Fikiri jinsi ambavyo Roho Mtakatifu anatupa uwezo wa kushuhudia.<br>2. Jadili umuhimu wa kutangaza Habari Njema ulimwenguni kwote.<br>3. Kama kikundi, jadili njia ambazo wanafunzi wanaweza kuwa washuhudiaji kwenye juma hili.<br>4. Tafuta njia ambazo toba ilifanyika miaka mingi iliyopita. | 1. Jadili umuhimu wa kazi ya Roho Mtakatifu.<br>2. Jadili umuhimu wa kukutana pamoja katika ushirika wa karibu kama Kanisa.<br>3. Tafuta kanisa linalokua kwa kasi na utaje sifa zake. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, kuwa mshuhudiaji kuna maanisha nini?<br>2. Je, kutubu kunamaanisha nini? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, kwanini Pentekoste ina umuhimu sana katika Kanisa la leo?<br>2. Jadili tofauti ya kwenda Kanisani na kuwa sehemu ya ushirika wa Kanisa? |

| | **A5 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Pili – Maisha ya Petro**<br>**Mada – Petro akiponya** | **A5 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Pili – Maisha ya Petro**<br>**Mada – Kumponya Kiwete** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 3: 1-16***<br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 3: 6***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Bwana Yesu ana uwezo wa kuponya magonjwa.<br>2. Anaweza kuyabadilisha maisha yetu tunapomwamini. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 3: 1-26***<br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 4: 10***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu anatuweka mahali sahihi katika wakati sahihi.<br>2. Nguvu ya Mungu ndiyo iliyo mponya yule kiwete na sio nguvu ya wale wanafunzi. |
| **TOA UTANGULIZI** | Petro na wanafunzi wengine wasingeweza kusahau ule mfano ambao Yesu aliwafundisha wa Msamaria Mwema na umuhimu wa “kuwapenda jirani zao” ***(Luka 10: 25-37)*** Walipomwona yule kiwete walijua kuwa walipaswa kufanya jambo ambalo Yesu angelifanya. | Moja ya mafundisho muhimu ya Bwana Yesu ilikuwa ni kuwajali wengine. Mara zote aliwaonesha wanafunzi wake upendo kwa kila mtu, hususani kwa wenye uhitaji. Aliwaambia kuwa atakapoondoka wangeweza kufanya mambo makubwa zaidi ya aliyokuwa ameyafanya. ***(Yohana 14: 12)*** |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Petro na Yohana wanaenda hekaluni kuomba.<br>2. Walikutana na mtu aliyekuwa kiwete tangu kuzaliwa kwake miaka arobaini iliyopita.<br>3. Yule mtu anaomba hela, lakini Petro anasema kuwa ana kitu kingine bora zaidi, angeweza kuponywa.<br>4. Akamsaidia yule mtu kusimama na kisha yule mtu aliyekuwa kiwete akaanza kurukaruka, na kutembea na kuingia hekaluni huku akimtukuza Mungu. Huu ulikuwa muujiza wa kwanza kwenye Kanisa la kwanza.<br>5. Watu walipokusanyika, Petro akaelezea kuwa mtu huyo alikuwa ameponywa kwa Jina la Yesu ambaye walimsulibisha na wala siyo kwa nguvu za Petro. ***(angalia mstari wa 16)***<br>6. Angalia msisitizo kuhusu imani ya yule mtu kwenye ***mstari wa 16.***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – A lame beggar is healed (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mara baada ya pentekoste, Petro na Yohana walienda hekaluni kuomba.<br>2. Walipomwona yule kiwete walijua jambo ambalo Bwana angelifanya.<br>3. Kwa imani, Petro akamsaidia yule mtu kusimama. Aliponywa mara ile, na alithibitisha kwa kutembea na kuruka huku na huku kwa furaha akiingia hekaluni huku akimtukuza Mungu.<br>4. Mara tu, aliponywa kabisa; ni kama miujiza mingi ambayo Yesu alifanya.<br>5. Nguvu ya Bwana Yesu sasa ilidhihirika kwa mitume wake kwa sababu ya ujio wa Roho Mtakatifu.<br>6. Tafakari mawazo makuu ya mahubiri ya Petro alipokuwa akielezea Yesu ni nani na nini anachoweza kufanya!<br>7. *Tafakari jinsi ambavyo Mungu anaweza kuwapa wanafunzi wake nguvu ya kuponya.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – A lame beggar is healed (I)** |
| **REJELEA SOMO** | 1. Fikiria kuhusu muujiza wa uponyaji na uhalisia kwamba sio wote wanaoponywa.<br>2. Jadili jinsi ambavyo Wakristo wanapaswa kushuhudia nyumbani (Yerusalemu yetu) kabla ya kwenda katika miisho ya nchi.<br>3. Tafuta Mkristo wa siku za leo ambaye amepata muujiza wa uponyaji.<br>4. Jadili mabadiliko ambayo Yesu anaweza kuyafanya katika maisha yetu tunapomwamini. | 1. Jadili namna ambavyo, tunapotenga muda ili kuwa na Yesu, maisha yetu ya kila siku na ushuhudiaji wetu unavyobadilika.<br>2. Panga muda wa kumwomba Mungu pamoja na Wakristo wengine ili Mungu awajaze nguvu zake na kuwapa fursa za kuhudumu.<br>3. Fikiria sababu za mabadiliko makubwa ya Petro tangu alipomkana Yesu. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, unafikiri ni kwanini Mungu hawaponyi watu wote?<br>2. Je, tunawezaje kumwamini Mungu katika maisha yetu ya kila siku? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Unajuaje upo sehemu ambayo Mungu anataka uwepo?<br>2. Tunawezaje kumsifu Mungu kwa kutusamehe dhambi zetu na kuyabadilisha maisha yetu? |

| | A5 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Maisha ya Petro<br>Mada – Petro Akishuhudia | A5 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Maisha ya Petro<br>Mada – Mbele ya Baraza |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 4: 1-22***<br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 4: 12***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Roho Mtakatifu alifanya mabadiliko makubwa katika maisha ya Petro.<br>2. Wakristo wanapaswa kuwa na msimamo kwa ajili ya Bwana. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 4: 1-31***<br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 4: 13***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alimpa Petro ujasiri na uwezo wa kushuhudia mbele ya viongozi wa dini.<br>2. Wakristo wanapaswa kuwa tayari kuwaambia wengine habari za Yesu kwa gharama yoyote. |
| TOA UTANGULIZI | Rudia kilichokuwa kimetokea kwenye somo lililopita. Wakumbushe wanafunzi kuwa, katika baadhi ya nchi, endapo utakuwa na msimamo kwa ajili ya Bwana Yesu, inaweza kupelekea mateso au hata kufungwa.<br>Katika tukio hili Petro na Yohana walipata mateso kutoka kwa viongozi wa kidini. | Petro alitoa mahubiri mazuri kwa mara nyingine tena. ***(sura ya 3)*** Idadi ya waamini ilikuwa takribani watu 5,000. ***(Mstari wa 4)*** Viongozi wa dini walidhani kwamba, Yesu aliposulubiwa, huo ungekuwa mwisho wa kuwa na wafuasi. Sasa wafuasi wake waliongezeka zaidi! |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Viongozi wa dini walisikia ujumbe wa Petro na hawakufurahishwa kwa kuwa kazi yao ilikuwa kufundisha watu, na pia Petro alikuwa anahubiri kuwa Bwana Yesu yu hai.<br>2. Petro na Yohana walikamatwa na kutiwa gerezani.<br>3. Siku iliyofuata walipelekwa mbele ya Baraza (mahakama ya kidini) kama ilivyokuwa kwa Yesu.<br>4. Walitaka kujua Petro alitumia nguvu gani kumfanya yule kiwete atembee.<br>5. Petro akawaambia ni kwa nguvu katika jina la Yesu. ***(mstari wa 10)***<br>6. Viongozi wa kidini walistaajabia ujasiri wa Petro na Yohana.<br>7. Wakawakataza kuhubiri habari za Yesu.<br>8. Petro akasema imewapasa kumtii Mungu na sio Baraza.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Peter and John arrested (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Petro na Yohana wanakamatwa.<br>2. Tazama umuhimu wa Baraza.<br>3. Petro aliwaambia kwa ujasiri kuwa nguvu ya Yesu ndiyo iliyomponya yule mtu liyekuwa kiwete, pia akaeleza kuwa Yesu pekee ndiye Mwokozi. ***(mstari 12)***<br>4. Baraza lilishangazwa na ujasiri wa Petro na Yohana na wakatambua ni kwa sababu walikuwa pamoja na Yesu.<br>5. Wakawaamuru waache kuhubiri kwa jina la Yesu. Lakini Petro akawaambia imewapasa kumtii Mungu na wala sio Baraza.<br>6. Petro na Yohana wakaachiliwa wakaenda kwa wenzao na wakamwomba Mungu ili awape ujasiri wa kunena habari zake. Tazama jinsi maombi yao yalivyojibiwa kwa nguvu ya ajabu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Peter and John arrested (I)** |
| REJELEA SOMO | 1. Andika kwa kifupi mambo muhimu ya imani ya Ukristo ambayo inafaa kuwa msingi. Kumbuka kuwa Bwana Yesu ni msingi wa Imani ya Mkristo. ***(Angalia mstari wa 12)***<br>2. Fanya utafiti kuhusu Mkristo anayefahamika aliyesimia imani yake kwa mfano Eric Liddell. | 1. Jadili namna ambavyo unaweza kuimarika zaidi katika imani na ushuhudiaji.<br>2. Tafiti kazi za shirika la Opens Doors au Barnabas Trust ili kujua jinsi ambavyo Wakristo wanaweza kushinda katika maeneo yenye mateso. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, ni mambo gani yanatuzuia kuwaambia wengine Habari za Yesu?<br>2. Je, inamaanisha nini kwa mwamini kuwa 'jiwe lililo hai'? ***(1 Petro 2: 4 & 5)*** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, tunawezaje kumtegemea Roho Mtakatifu kutusaidia katika ushuhudiaji?<br>2. Je, ni kwa namna gani upinzani juu ya Injili ya Yesu unaweza kutusaidia kukua? |

| | A5 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Maisha ya Petro<br>Mada – Petro gerezani | A5 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Maisha ya Petro<br>Mada – Gerezani |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Matendo 12: 1-19***<br>**Mstari Muhimu:** ***1Yohana 5: 14***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mateso ni jambo ambalo linaweza kuwaathiri watu wa Mungu.<br>2. Biblia inatufundisha kuwa Mungu anatupenda na anajua mambo yaliyomema kwetu. | **Neno la Biblia:** ***Matendo 12: 1-19***<br>**Mstari Muhimu:** ***1 Yohana 5: 5***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kuna umuhimu wa kumwamini Mungu kama Petro alivyofanya hata kwenye wakati mgumu.<br>2. Mungu anafanya yasiyowezekana na mengine anatuachia. |
| TOA UTANGULIZI | Bwana Yesu alisema, kama ulimwengu ulivyomchukia Yeye, ungewachukia pia Mitume na watu wote wa Mungu. ***(Yohana 15: 18)***. Yesu alipokuwa mtoto, Mfalme Herode alijaribu kumwua. Wakati huu sasa Herode Mwingine, aliyekuwa mjukuu wa Mfalme Herode, anataka kufanya jambo lile lile kwa Petro. | Kwa mara nyingine Petro anawekwa gerezani kwa kwa sababu ya imani na mahubiri yake. Lazima alikuwa na imani kubwa kwani alipata usingizi akiwa gerezani, usiku kabla ya kesi yake. Je, Petro alikuwa amegundua kweli ya maneno ambayo baadaye aliyaandika? ***(1 Petro 5: 7)*** |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mfalme Herode alimuua Yakobo na alipoona kuwa amewafurahisha Wayahudi akamkamata Petro.<br>2. Petro yupo gerezani kwa mara nyingine, akisubiri hukumu yake mbele za watu.<br>3. Kanisa likakutana kuomba.<br>4. Usiku ule kabla ya hukumu, malaika akamsaidia Petro kutoka gerezani.<br>5. Alikwenda kwenye nyumba ambayo rafiki zake walikuwa wakiomba.<br>6. Kijakazi aliyefungua mlango akawaambia kuwa Petro alikuwa mlango, lakini hakuna aliyemwamini.<br>7. Mwishowe wakatambua kuwa Mungu alikuwa amejibu maombi yao.<br>8. *Fikiria umuhimu wa ushirika wa kweli kati ya Wakristo.*<br>9. *Fikiria jinsi gani tunatakiwa kuomba kila mara, tukitarajia Mungu kujibu maombi yetu na kuyakubali mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yetu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Peter's miraculous escape from prison (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Kanisa likasikitishwa na lile jambo la Petro kukamatwa na likamwomba Mungu kwa juhudi kwa ajili yake.<br>2. Petro alilindwa na askari 16 na alifungwa kwa minyororo katikati ya askari wawili.<br>3. Malaika akatokea, akamwamsha Petro na kumfungua minyororo na akamwongoza nje ya gereza. Kwa muujiza Petro akawa huru.<br>4. Petro akatambua kuwa ni Bwana alikuwa amemwokoa.<br>5. Aligundua kuwa Kanisa lilikuwa likimwombea lakini hawakuamini kwa haraka kuwa Mungu anaweza kufanya yasiyowezekana.<br>6. Ni wazi kuwa Mungu alikuwa na kazi zaidi kwa ajili ya Petro. Mungu akaingilia kati kwani muda wa Petro kufa ulikuwa bado haujafika.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Peter's miraculous escape from prison (I)** |
| REJELEA SOMO | 1. Jadili kwanini ni vigumu kwa Wakristo kuomba mara kwa mara?<br>2. Jadili kuhusu nyakati ambazo umefahamu kuwa haukuwepo kwenye mapenzi ya Mungu.<br>3. Tafuta mistari miwili ya Biblia inayohusu muongozo wa Mungu na uwashirikishe watu wa kundi lako. | 1. Fikiria kuhusu umuhimu wa kumwomba Mungu katika nyakati ngumu.<br>2. Fikiri namna tunavyopaswa kuomba huku tukitarajia na kuamini kuwa Mungu atajibu.<br>3. Mwombe rafiki wa karibu au ndugu akupe mfano wa jinsi ambavyo Mungu alijibu maombi yao na uwashirikishe wengine. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kwanini wakati mwingine njia za Mungu zinaonekana kama siri (wengine wanaponywa wengine hawaponywi)?<br>2. Je, tunawezaje kutambua mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yetu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Kwanini mara kwa mara tunakuwa na mashaka kuwa Mungu atajibu maombi yetu kama tunayomwomba?<br>2. Je! Kwa njia gani tunajua kuwa nguvu za Mungu ni kubwa zaidi ya nguvu zetu? |

| | A6 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Safari za Ibrahimu<br>Mada – Kumtumaini Mungu | A6 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Safari za Ibrahimu<br>Mada – Wito wake |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 12: 1-9***<br>**Mstari Muhimu:** ***Waebrania 11: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Abramu alikuwa mtu wa imani: Alimwamini Mungu hata wakati alipokuwa hajui mahali ambapo Mungu alikuwa anamwongoza.<br>2. Mungu anapotuita, kama alivyomwita Abramu, tunatakiwa kumwamini, kumfuata na kumtii. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 11:27-32; Mwanzo 12:1-9***<br>**Mstari Muhimu:** ***Matendo 7: 2-4***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Abramu alikuwa mtu wa imani: Alimwamini Mungu hata wakati alipokuwa hajui mahali ambapo Mungu alikuwa anamwongoza.<br>2. Mungu anapotuita, kama alivyomwita Abramu, tunatakiwa kumwamini, kumfuata na kumtii. Kwa kweli, tunapaswa kumkabidhi maisha yetu. |
| **TOA UTANGULIZI** | • Waulize wanafunzi kama walishawahi kuhama kwenda kwenye shule mpya. Je, walikumbana na changamoto zipi? (Unaweza kujadili kubadilika kwa ratiba, mipango mbalimbali ya safari, kupata marafiki wapya na kukutana na walimu wapya).<br>• Uliza kama kuna mmoja wa wanafunzi ambaye alishawahi kuhama kwenda kwenye nyumba mpya. Je, jambo hili lilileta changamoto zipi? Kwa Abramu na familia yake, inawezekana changamoto zao mpya zilijumuisha lugha ya tofauti, chakula, hali ya hewa na utamaduni mpya pamoja na kuwa mbali na marafiki zao wa nyumbani. | Majadiliano ya kutembea (Walking debate). Waambie wanafunzi wafikirie kuwa wanaenda safari ndefu katika nchi ambayo hawajawahi kufika hapo awali, na mpango ni kufanya makazi mapya katika nchi hiyo. Je, jambo hili lilileta changamoto zipi? (Kwa Abramu na familia yake, inawezekana changamoto zao mpya zilijumuisha lugha ya tofauti, chakula, hali ya hewa na utamaduni mpya pamoja na kuwa mbali na marafiki zao wa nyumbani.)<br>Andika kila mojawapo ya maneno haya katika karatasi ya A4: SINA UHAKIKA; NINAOGOPA; NINA FURAHA; NINA MAWAZO; NINA MASHAKA. Bandika karatasi hizo katika ukuta wa darasa, kwenye sehemu tofauti. Waambie wanafunzi watembee na kwenda kusimama kwenye karatasi inayoelezea vizuri zaidi hisia zao kuhusu hali iliyoelezewa hapo juu. Kisha jadili uchaguzi wao: kwanini walihisi hivyo? |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu aliongea na Abramu na kumwambia atoke yeye na familia yake aende nchi nyingine, atakayomwonesha. Jambo hili halikuwa rahisi. Usafiri katika nyakati za Abramu ulikuwa ni wa shida na wa mwendo wa polepole. Pia alikuwa na mambo mengi sana ya kuandaa na watu wa kwenda naye.<br>2. Mungu aliweka ahadi ya pekee ya kumbariki Abramu na kuifanya familia yake kuwa taifa kubwa. Kupitia taifa hili kubwa, watu wengine wote duniani wangebarikiwa.<br>3. Abramu aliondoka na mpwa wake, Lutu na Sarai mkewe. Walichukua vitu vyao vyote. Abramu alikuwa na umri wa miaka 75!<br>4. Baada ya kusafiri kwa muda fulani, Bwana akamtokea Abramu wakiwa kwenye eneo linaloitwa Shekemu. Akamwambia Abramu kuwa ataipa familia yake nchi ile.<br>5. Abramu akajenga madhabahu na kumwabudu Bwana. Kisha akaendelea na safari hadi kwenye vilima katikati ya Ai na Betheli, akaweka hema yake pale. Akajenga madhabahu tena na kumwabudu Mungu. Akaendelea na safari tena kuelekea jangwa la Negebu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Abram moves to Canaan (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu aliongea na Abramu na kumwambia atoke yeye na familia yake aende nchi nyingine. Jambo hili halikuwa rahisi. Usafiri katika nyakati za Abramu ulikuwa ni wa shida na wa mwendo wa polepole. Pia alikuwa na mambo mengi sana ya kuandaa na watu wa kwenda naye.<br>2. Mungu aliweka ahadi ya pekee ya kumbariki Abramu na kuifanya familia yake kuwa taifa kubwa. Kupitia taifa hili kubwa, watu wengine wote duniani wangebarikiwa.<br>3. Abramu aliondoka na mpwa wake, Lutu na Sarai mkewe. Walichukua vitu vyao vyote. Abramu alikuwa na umri wa miaka 75!<br>4. Baada ya kusafiri kwa muda fulani, Bwana akamtokea Abramu wakiwa kwenye eneo linaloitwa Shekemu. Akamwambia Abramu kuwa ataipa familia yake nchi ile.<br>5. Abramu akajenga madhabahu na kumwabudu Bwana. Kisha akaendelea na safari hadi kwenye vilima katikati ya Ai na Betheli, akaweka hema yake pale. Akajenga madhabahu tena na kumwabudu Mungu. Akaendelea na safari tena kuelekea jangwa la Negebu.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Abram moves to Canaan (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Chora ramani inayohusu safari ya Abramu kutoka Harani hadi Betheli na uoneshe jina la kila eneo lililotajwa kwenye habari hii. Kumbuka kuonesha ule mti mkubwa wa More na madhabahu mbili ambazo Abramu alijenga ili kumwabudu Bwana. | Sasa orodhesha maneno ambayo tunaweza kuyatumia kuonesha hisia ya Abramu juu ya wito wa Mungu wa kuhamia nchi nyingine, kulingana na habari tuliyosoma leo kwenye Biblia. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Japokuwa jambo hili halikuwa rahisi, Abramu alitii Mungu alipomwambia aanze safari yake. Je, jambo hili linatuonesha nini kuhusu tabia ya Abramu?<br>2. Je, ni kwa namna gani imani yetu kwa Mungu inaathiri mienendo yetu ya kila siku, hata katika hali tusizoelewa kikamilifu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Katika makundi ya watu wawili au watu watatu, jadili: Abramu alimtii Mungu. Jambo hili linatufundisha nini kuhusu mtazamo wa Abramu kumhusu Mungu?<br>2. Fikiria kuhusu hali ambazo kumtii Mungu inawezea kuwa changamoto. Habari ya Abramu inatufundisha nini kuhusu namna tunavyopaswa kuenenda, hata wakati ambapo tunajihisi kuwa hatuna uhakika, tuna hofu au mashaka? |

| | A6 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Safari za Ibrahimu<br>Mada – Chaguzi | A6 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Safari za Ibrahimu<br>Mada – Chaguo Lake |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 13: 1-18***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mithali 3: 5 & 6***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Ni muhimu kufanya maamuzi mazuri kwenye maisha yetu.<br>2. Tunapaswa kumwomba Mungu atusaidie kufanya maamuzi mazuri. Tunapaswa kuomba uongozi wake. Tunapaswa pia kukumbuka kumshukuru Mungu na kumwabudu. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 13: 1-18; Mwanzo 14: 1-16***<br>**Mstari Muhimu:** ***Yoshua 24: 15***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Abramu alitafuta uongozi na msaada wa Mungu, pia alimshukuru.<br>2. Tunapaswa kumkiri Mungu katika kila jambo tunalolifanya, huku tukitafuta msaada na uongozi wake na kumpa sifa zote na heshima kwa baraka katika maisha yetu. |
| TOA UTANGULIZI | • Sote tunafanya chaguzi na maamuzi kila siku. Waombe wanafunzi watoe mifano ya maamuzi madogo madogo ya kila siku na kisha watoe baadhi ya mifano ya maamuzi makubwa yaliyobadilisha maisha yao. Andika majibu hayo kwenye orodha mbili katika karatasi.<br>• Mpe karatasi kila mmoja. Upande mmoja wanapaswa kuchora picha inayoonyesha uamuzi mdogo ambao wameufanya siku za karibuni. Upande mwingine wanatakiwa wachore picha inayoonesha tumaini, ndoto au matamaino waliyonayo kwa wakati ujao. Kwa vikundi vya watu wachache wanaweza kushirikishana na kujadili picha zao. | Kumtumikia Mungu ni uamuzi.<br>Je, tunaweza kuona tofauti gani kwenye Maisha ya watu walioamua kumtumikia Mungu?<br>Orodhesha majibu kwenye karatasi na uendelee kuyakumbuka kadiri tunavyoendelea kujifunza kwa kifupi kuhusu maisha ya Abramu katika somo hili. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Abramu alirudi sehemu aliyowahi kuweka hema yake, katikati ya Betheli na Ai. Alikuwa amemjengea Bwana madhabahu pale na alienda kuomba na kuliitia jina la Bwana.<br>2. Abramu alitakiwa kufanya maamuzi. Katika nchi ile kulikuwa na watu wengi sana na waligombania ile ardhi. Ardhi haikutosha kwa kila mtu, hivyo ukafika muda wa Abramu kutengana na mpwa wake, Lutu na kuishi katika eneo tofauti.<br>3. Abramu akampa Lutu nafasi ya kuchagua eneo ambalo angependa kuishi.<br>4. Lutu alichagua bonde lenye rutuba na maji kando ya mto Yordani na kuamua kuishi karibu na miji.<br>5. Abramu akaishi kwenye nchi ya Kanaani.<br>6. Baada ya Lutu kuondoka, Bwana aliongea na Abramu na kumwahidi ardhi yote ambayo aliweza kuiona pande zote: kaskazini, kusini, mashariki na magharibi.<br>7. Mungu alimwahidi Abramu kuwa atakuwa na watoto wengi sana na nchi ile itakuwa yao.<br>8. Abramu aliamua kuishi karibu na mialoni ya Mamre, nayo ni miti iliyoko Hebroni. Akajenga madhabahu pale na kumwabudu Bwana.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Abram and Lot separate (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Abramu alikuwa na uamuzi wa kufanya. Katika nchi ile kulikuwa na watu wengi sana na waligombania malisho ya wanyama. Hivyo ukafika muda wa Abramu kutengana na mpwa wake, Lutu na kuishi katika eneo tofauti.<br>2. Abramu akampa Lutu nafasi ya kuchagua eneo ambalo angependa kuishi.<br>3. Lutu alichagua bonde lenye rutuba na maji kando ya mto Yordani na kuamua kuishi karibu na miji.<br>4. Abramu akaishi kwenye nchi ya Kanaani.<br>5. Baada ya Lutu kuondoka, Bwana aliongea na Abramu na kumwahidi ardhi yote ambayo aliweza kuiona pande zote. Mungu alimwahidi Abramu kuwa atakuwa na watoto wengi sana na nchi ile itakuwa yao.<br>6. Abramu aliamua kuishi karibu na mialoni ya Mamre, nayo ni miti iliyoko Hebroni. Akajenga madhabahu pale na kumwabudu Bwana.<br>7. Abramu alikuwa akiishi katika kipindi cha ugomvi. Maadui Sodoma, kule alipoishi Lutu, walivamia mji na walimteka Lutu pamoja na watu wengine na mali zao.<br>8. Abramu aliposikia hayo, alikwenda na jeshi kuwashambulia maadui na kuwarejesha waliokuwa wametekwa. Abramu aliwashinda watekaji. Asingeweza kukubali malipo kutoka kwa Mfalme wa Sodoma kwani ni Mungu ambaye alimpa ushidi dhidi ya maadui.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Abram and Lot separate (I)** |
| REJELEA SOMO | Tengeneza kichwa cha habari cha kwenye gazeti na ripoti fupi katika ukurasa wa mbele kutoka kwenye habari ya somo la leo. Ripoti hii inatakiwa kuwa na dondoo muhimu za habari.<br>Kazi inaweza kukamilishwa kwenye makundi madogo au ya watu wawili wawili. Ripoti hii inaweza kuonyeshwa na kujadiliwa. | Soma Mstari Muhimu ***Yoshua 24: 15***. Kutokana na ulivyojifunza kwenye funzo hili, Abramu alionesha kwa namna gani kuwa yeye ni mtumishi wa Mungu?<br>Rejelea orodha ya tabia za mtumishi wa Mungu, kama ilivyoelezewa mwanzoni mwa somo hili. Je,<br>kuna mambo ambayo sasa ungependa kuyaongeza au kuyabadilisha? Je, kumtumikia Mungu kunatakiwa kuleta mabadiliko gani kwenye maisha yetu leo? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Abramu alimuhusisha Mungu kwenye chaguzi na maamuzi yake na Mungu akambariki. Fikiria kumwomba Mungu akuongoze unapofanya maamuzi muhimu katika maisha yako. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>Mpe kila mwanafunzi kijikaratasi. Wape changamoto ya kufikiria kuhusu njia moja ambayo wanaweza kumtumikia Mungu kwa uaminifu zaidi. Wanaweza kuandika ombi binafsi kutokana na ujumbe uliopo kwenye kijikaratasi na kwenda nao nyumbani kama kumbukumbu ya somo. |

| | **A6 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Tatu – Safari za Ibrahimu**<br>**Mada – Ahadi za Mungu** | **A6 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Tatu – Safari za Ibrahimu**<br>**Mada – Ujasiri wake** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 17: 1-8; 18: 1-15; 21: 1-5***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 1: 21***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Pamoja na kuwa Abramu alijaribu kufanya mambo kwa namna yake mwenyewe, Mungu hakumwacha.<br>2. Mungu alimhakikishia Abramu kuwa atakuwa baba wa mataifa mengi. Ilimaanisha baraka sio tu kwa Abramu bali kwa watu wote katika historia.<br>3. Kuna wakati tunaweza kupata wasiwasi kuhusu ahadi za Mungu kwa sababu zinaonekana kuwa za ajabu. Tunaweza kujaribu kutengeneza mambo peke yetu. Somo hili linatuhamasisha kuamini ahadi za Mungu na kusubiria zitimie. | **Neno la Biblia:** ***Mwanzo 15: 1-7; 17: 1-19; 18: 1-15***<br>**Mstari Muhimu:** ***Mwanzo 18: 14***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alimuahidi Abramu kuwa atakuwa na mtoto ambaye atakuwa mrithi wake. Abramu alimwamini Mungu, lakini yeye na mkewe walikuwa wazee na walikuwa hawajawahi kupata watoto. Wakajaribu kutengeneza mambo peke yao.<br>2. Mungu kamwe hakuwaacha Abramu na Sarai. Mungu akahakikisha ahadi yake kuwa Abramu atakuwa baba wa mataifa mengi. Ilimaanisha baraka sio tu kwa Abramu bali kwa watu wote katika historia.<br>3. Kuna wakati tunaweza kupata wasiwasi kuhusu ahadi za Mungu kwa sababu zinaonekana kuwa za ajabu. Somo hili linatuhamasisha kuamini ahadi za Mungu na kusubiria zitimie. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize wanafunzi kama walishawahi kutoa ahadi. Je, yupo mwanafunzi yeyote ambaye amewahi kutoa ahadi kwa mwanafunzi mwenzake katika kundi hilo? Andika orodha ya majibu haya kwenye karatasi. Wakati mwingine watu hawatimizi ahadi zao. Je, ni kwa sababu gani? (Jadili na kundi lote) Somo hili linatufundisha kuwa Mungu anatimiza ahadi zake, hata inapoonekana kama hataweza kutimiza. | Andika kwenye ubao au karatasi, orodha ya ahadi zinazotolewa na watu leo (kiapo cha ndoa, kiapo cha jeshini, makubaliano ya kisheria, makubaliano ya malipo, n.k.)<br>Jadili kiwango ambacho ahadi hizo zaweza kutimizwa au kuvunjwa. Funzo la leo linatufundisha kuwa Mungu anatimiza ahadi zake. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimwahidi Abramu kuwa atakuwa na watoto wengi.<br>2. Abramu na Sarai mkewe walikuwa wazee na walijaribu kutengeneza mambo wenyewe.<br>3. Pamoja na hivyo, Mungu hakuvunja ahadi yake. Bali aliwahakikishia tena Abramu na Sarai. Akawapa majina mapya kama ishara ya ahadi – wataitwa Ibrahimu na Sara.<br>4. Mungu akamwambia Ibrahimu kuwa atakuwa baba wa mataifa mengi. Akaahidi kuwa atampa Ibrahimu na uzao wake ardhi ile na kwamba atakuwa Mungu wao.<br>5. Watu watatu walikuja kumtembelea Ibrahimu. Ibrahimu alikuwa mkarimu sana kwao.<br>6. Bwana akamwambia Ibrahimu kuwa Sara atapata mwana wa kiume muda kama huo mwakani. Sara alicheka aliposikia hayo, kwa sababu yeye na Ibrahimu walikuwa wazee kuweza kupata watoto.<br>7. Mungu alitimiza ahadi yake na Sara akapata mwana wa kiume.<br>8. Ibrahimu na Sara walimwita mtoto wao Isaka, jina linalomaanisha “kicheko” kwa sababu Mungu alikuwa ametimiza ahadi isiyoaminika kwao na kuwapatia furaha kubwa katika uzee wao.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Abraham and the three strangers (I)** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na uelezee:**<br>1. Mungu alimwahidi Abramu kuwa atakuwa na Watoto wengi.<br>2. Abramu na Sarai mkewe walikuwa wazee na walijaribu kutengeneza mambo wenyewe.<br>3. Mungu kamwe hakuwaacha. Alithibitisha ahadi ile. Mungu akawapa Abramu na Sarai majina mapya. Sasa wataitwa Ibrahimu na Sara, ikiwa ni kumbukumbu ya ahadi yake.<br>4. Mungu akamwambia Ibrahimu kuwa atakuwa baba wa mataifa mengi. Akaahidi kuwa atampa Ibrahimu na uzao wake ardhi ile na kwamba atakuwa Mungu wao.<br>5. Watu watatu walikuja kumtembelea Ibrahimu. Ibrahimu alikuwa mkarimu sana kwao.<br>6. Bwana akamwambia Ibrahimu kuwa Sara atapata mwana wa kiume muda kama huo mwakani. Sara alicheka aliposikia hayo, kwa sababu yeye na Ibrahimu walikuwa wazee kuweza kupata watoto.<br>7. Mungu alitimiza ahadi yake na Sara akapata mwana wa kiume!<br>8. Ibrahimu na Sara walimwita mtoto wao Isaka, jina linalomaanisha “kicheko” kwa sababu Mungu alikuwa ametimiza ahadi isiyoaminika kwao na kuwapatia furaha kubwa katika uzee wao.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Abraham and the three strangers (I)** |
| **REJELEA SOMO** | Soma Mstari Muhimu. Tumia swali lililopo kwenye mstari huu kutengeneza alamisho ya kitabu/ kifaa cha kutia alama kwenye kitabu (bookmark kwa Kiingereza). Kila wakati unapoangalia alamisho hiyo ukumbuke kuwa Mungu anatimiza ahadi zake, hata kama zitaonekana ni za ajabu kwetu. | Kwenye vikundi vidogo: Tunajifunza nini kuhusu tabia ya Mungu, Ibrahimu na Sara kwenye somo hili? Wanafunzi waandike mawazo yao kwenye karatasi na kisha wajadili kwa pamoja. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, unamwamini Mungu?<br>2. Je, unaamini ahadi anazozitoa kwenye Neno Lake?<br>3. Je, ni kwa namna gani somo hili litaimarisha imani yako kwa Mungu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:**<br>1. Je, kuna mambo kwenye maisha yako ambayo unafikiri kuwa ni magumu kwa Mungu?<br>2. Je, ni jambo gani ulilojifunza kwenye funzo hili ambalo linakutia moyo kumwamini Mungu katika kila sehemu ya maisha yako? |

<table>
<tr><th></th><th>A6 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Safari za Ibrahimu<br>Mada – Jaribio la Upendo</th><th>A6 – RARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Safari za Ibrahimu<br>Mada – Changamoto</th></tr>
<tr><td></td><td>Neno la Biblia: Mwanzo 22: 1-14<br>Mstari Muhimu: Yohana 1: 29<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Mungu alimjaribu Ibrahimu. Alimwambia Ibrahimu amtoe sadaka mwanawe wa pekee. Ibrahimu alimtii Mungu na kumwamini kabisa.<br>2. Mungu ni Mpaji Mkuu: Alitoa sadaka iliyochukua nafasi ya Isaka.<br>3. Mungu alimtoa Bwana Yesu kuchukua nafasi yetu na kufa kama dhabihu ili kuondoa dhambi zetu.</td><td>Neno la Biblia: Mwanzo 22: 1-19<br>Mstari Muhimu: Waebrania 11: 17-19<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Mungu alimjaribu Ibrahimu. Wakati ambapo Mungu alimwambia Ibrahimu amtoe sadaka mwanawe wa pekee, Ibrahimu alimtii Mungu na kumwamini kabisa.<br>2. Mungu ni Mpaji Mkuu: Alitoa sadaka iliyochukua nafasi ya Isaka.<br>3. Mungu alijua kuwa Ibrahimu alikuwa amemtii na alikuwa tayari kumpa kila kitu, hivyo basi akathibitisha ahadi yake kwa mara nyingine.<br>4. Mungu alimtoa Bwana Yesu kuchukua nafasi yetu na kufa kama dhabihu ili kuondoa dhambi zetu.</td></tr>
<tr><td>TOA UTANGULIZI</td><td>Wakati mwingine tunatumia majaribio ili kujua mambo kuwahusu watu. Tengeneza orodha ya mitihani/majaribio ambayo watu hufanya (majaribio ya udereva, mitihani ya shule, mitihani ya muziki, mitihani ya kuona na kusikia, n.k.) Majaribio haya huonesha kitu kuhusu ufahamu, uelewa, uwezo wa mwili na tabia za watu. Katika habari hii, Mungu alitumia jaribio ili kuona kama kweli Ibrahimu anamwamini.</td><td>Je, kuna jambo au mtu katika maisha yako ambaye hauwezi kuishi bila yeye?<br>Kwa Ibrahimu, mwanawe Isaka angekuwa mmoja wa watu hao. Ibrahamu alisubiri kwa muda mrefu sana kumpata Isaka. Je, Ibrahimu angejihisi nini kama angempoteza Isaka?</td></tr>
<tr><td>KAMILISHA</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Mungu alimwambia Ibrahimu amtoe mwanaye wa pekee Isaka, ambaye Mungu aliamuahidi, kama sadaka ya kuteketezwa.<br>2. Ibrahimu alitii maelekezo ya Mungu. Ibrahimu alisafiri kwa siku tatu kufika sehemu ambayo Mungu alimwambia aende.<br>3. Isaka alipouliza kuhusu sadaka ilipo, Ibrahimu akajibu kuwa Mungu atajipatia sadaka. Hii inaonesha kuwa Ibrahimu alikuwa na imani kubwa kwa Mungu.<br>4. Ibrahimu alikuwa mtiifu kwa Mungu kikamilifu. Alikuwa yupo tayari kutoa kila kitu kwa Mungu na kumtoa sadaka mwanawe wa thamani.<br>5. Mungu akamwita Ibrahimu na kumwambia asimdhuru mwanawe Isaka.<br>6. Hakika Mungu akatoa sadaka iliyochukua nafasi ya Isaka: Mwanakondoo.<br>7. Mungu alithibitisha ahadi yake kwa Ibrahimu ya kuwa atauzidisha uzao wake na hakuna atakayeweza kuwahesabu. Pia aliahidi kupitia wao atawabariki mataifa yote ulimwenguni.<br>8. Mungu alimtuma Mwanae wa pekee kuchukua sehemu yetu kama “Mwanakondoo wa Mungu”. Kupitia Bwana Yesu, Mungu anatubariki kwa wokovu ikiwa tunamwamini.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Somo la Nne.<br>Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Abraham and Isaac (I)</td><td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na uelezee:<br>1. Mungu alimwambia Ibrahimu amtoe mwanaye wa pekee Isaka, ambaye Mungu aliamuahidi, kama sadaka ya kuteketezwa.<br>2. Ibrahimu alitii maelekezo ya Mungu. Ibrahimu alisafiri kwa siku tatu kufika sehemu ambayo Mungu alimwambia aende.<br>3. Isaka alipouliza kuhusu sadaka ilipo, Ibrahimu akajibu kuwa Mungu atajipatia sadaka. Hii inaonesha kuwa Ibrahimu alikuwa na imani kubwa kwa Mungu.<br>4. Ibrahimu alikuwa mtiifu kwa Mungu kikamilifu. Alikuwa yupo tayari kutoa kila kitu kwa Mungu na kumtoa sadaka mwanawe wa thamani.<br>5. Mungu akamwita Ibrahimu na kumwambia asimdhuru mwanawe Isaka.<br>6. Hakika Mungu akatoa sadaka iliyochukua nafasi ya Isaka: Mwanakondoo.<br>7. Mungu alithibitisha ahadi yake kwa Ibrahimu ya kuwa atauzidisha uzao wake na hakuna atakayeweza kuwahesabu.<br>8. Mungu alimtuma Mwanae wa pekee kuchukua sehemu yetu kama “Mwanakondoo wa Mungu”. Kupitia Bwana Yesu, Mungu anatubariki kwa wokovu ikiwa tunamwamini.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Funzo la Nne.<br>Onesha: Tafuta kwenye tovuti ya FBI – Abraham and Isaac (I)</td></tr>
<tr><td>REJELEA SOMO</td><td>Mstari Muhimu unatufundisha kuwa Bwana Yesu ni sadaka kamilifu, Mwanakondoo wa Mungu, anayeondoa dhambi za ulimwengu. Je, umemwamini Mungu na kumkubali Bwana Yesu kama Mwokozi wako?</td><td>“Katika mlima wa BWANA itapatikana” ni jina ambalo Ibrahimu aliliita eneo ambalo matukio tuliyoyaona kwenye funzo la leo yalitokea.<br>Je, ni kwa namna gani Mungu ametupa mahitaji yetu?</td></tr>
<tr><td>LIISHI SOMO</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>Ibrahimu alimwamini Mungu kikamilifu na kumtii, na kwa hili Mungu akambariki sana. Je, tunawezaje kuufuata mfano wa Ibrahimu?</td><td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto:<br>Ibrahimu alimwamini Mungu na kumtii, hata wakati alipojaribu imani yake. Je, tunawezaje kuufuata mfano wake?</td></tr>
</table>

## Maelekezo ya waalimu wanaposahihisha masomo

**Masomo ya Daraja la Tatu**

- Wanafunzi hawawezi kukamilisha masomo haya bila kurejelea Biblia na wanaweza kulazimika kurejelea kifungu kimoja au zaidi vya Maandiko ya Biblia.
- Maswali yapo katika namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na jedwali la maneno, maneno yaliyokosekana, n.k.
- Masomo yametegenezwa kujibiwa kwa toleo la Biblia ya Kiswahili, Union Version iliyochapishwa kama “BIBLIA Maandiko Matakatifu”.
- Lengo letu ni kwamba wanafunzi wote, waweze kujibu maswali kwa kutumia Biblia yoyote waliyo nayo.
- Alama ishirini zimetengwa kwa kila wiki ambapo kiwango cha juu kwa mwezi ni 80, pale masomo yanapokuwa ni sahihi kabisa.
- Daraja la tatu – Kwa kawaida na kama inavyooneshwa, alama 1 kwa kila jibu linalohitajika.

**Mafunzo ya Daraja la Nne**

- Masomo haya ni ya ngazi ya juu ya yale masomo ya Daraja la Tatu.
- Maswali ni ya kiwango cha juu na majibu ya kina zaidi yanahitajika.
- Alama ishirini kwa wiki na alama 80 kwa mwezi, wakati masomo yakiwa ni sahihi kabisa na maswali yana majibu kamili.

**VIDOKEZO VYA KUSAHIHISHA**

Walimu wanatakiwa, kwanza:

- Kukagua vizuri kila somo na kusahihisha majibu yaliyo sahihi au yasiyo sahihi.
- Toa alama kama ilivyoelekezwa.
- Kila mara, tumia kalamu ya rangi tofauti kusahihisha na kuweka ALAMA YA VEMA (✔) kwenye kila jibu sahihi.
- Weka au andika jibu sahihi panapostahili, na rekebisha makosa yoyote ya maandishi (spelling errors), lakini HAKUNA alama zinazoondolewa kwa ajili ya kosa hili.
- Toa alama chache kwa kila jibu ambalo sio sahihi kabisa.
- Jumlisha alama za mwezi na uandike kwenye nafasi iliyotolewa kwenye ukurasa wa mwisho.

Ni muhimu kuwa mkarimu kama uwezavyo ili kuwatia moyo watoto/ wanafunzi wafanye masomo ya Biblia. Kila mwezi, ni muhimu kwa mwalimu kuandika maneno ya kutia moyo kwenye nafasi iliyowekwa kwa kila mtoto anayemfundisha. Unaweza kuandika kuhusu kupaka rangi vizuri, kufanya kazi safi, alama alizopata mtoto, uelewa wa masomo wa mtoto na kadhalika.
Tunajaribu kutoa mawazo tofauti kama iwezekanavyo. Maswali, maoni, maneno ya kutia moyo na kadhalika, yote yanaweza kutumiwa kuleta utofauti. Kama maoni au usemi mmoja unatumika kila mwezi, watoto watauona hauna maana tena.

**Daraja la Tatu**

**Maoni ya jumla**

"Kazi njema! Ni wazi kwamba umesoma maswali kwa umakini sana. Nilipenda sana jibu lako la swali la mwisho ambalo lilikuwa limeandikwa vizuri. "
"Habari Yusufu. Hongera kwa kufanya kazi kwa bidii sana! Ilikuwa vizuri kwamba uliweza kujibu takriban majibu yote. Nimekujazia yale ambayo hayajakamilika."

**Maoni ya kiroho**

"Musa alikuwa na wakati mgumu na wana wa Israeli, lakini Mungu hakumwacha kutatua matatizo yote peke yake."
"Yusufu hakusahau kuwa baba yake alikuwa amemfundisha kumpenda Mungu. Alikumbuka hili hata alipokuwa mbali na nyumbani.”
"Bartimayo alikuwa ameazimia kufika kwa Bwana Yesu. Hakujutia uamuzi wake kwani sasa alikuwa na uwezo wa kuona na sasa alijua kuwa Bwana Yesu alikuwa mtu wa pekee sana."

**Daraja la Nne.**

**Maoni ya jumla**

"Seti nyingine nzuri sana ya masomo. Unaonekana kuwa na ufahamu mzuri wa habari hizi za Biblia na ninatumaini kuwa umezifurahia. Asante kwa kutumia muda wako kufanya masomo kwa umakini. Ungeliweza kufanya masomo haya kwa haraka haraka, kwahiyo ninathamini juhudi zako zote."
"Neema, umejitahidi sana. Nadhani kwa majibu uliyoyatoa, pengine haukuweza kuelewa habari vizuri. Labda ungejaribu kuisoma tena."

**Maoni ya kiroho**

"Mifano ya Biblia wakati mwingine huitwa habari za kidunia zenye maana ya kimbingu, au maana ya ndani zaidi. Je! Unaweza kufikiria kuna maana gani ya kina katika mfano kwenye Funzo la Tatu?"
"Stefano alikufa kifo cha kikatili na bado hakuogopa kufa, kwa vile alijua kuwa Mungu bado anatawala kila jambo na alijua atakuwa na Bwana Yesu Mbinguni."

© Bible Educational Services 2019

www.besweb.com

Registered Charity UK 1186004

Toleo la 09/2020